*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo

## Maafisa ugani kupimwa kulingana na kazi zao



Uk. 4

**Serikali kuboresha huduma bora za afya kwa wananchi** Uk. 7

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00043 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Desemba 20 - 26, 2023 |



**KIMATAIFA** Uk. 19

## Tetemeko la ardhi laua watu 111 China



## SALAMU ZAO...

- Simba yaitungua Wydad

Na Mwandishi Wetu

NANI alisema haiwezekani, nani alimkatia Onana tamaa? Simba wametakata Dar.

Ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wydad Casablanca umefufua matumaini ya Simba kwenda robo fainali ya Klabu Bingwa Afrika. Uk. 24



### MAGEUZI MAKUBWA NHIF:


# Rais Dk. Samia ashusha gharama kuchuja damu





**Haemodialysis** bei ya sasa ni Sh. 240,000 wakati bei iliyoboreshwa itakuwa Sh. 200,000. **Erythropoietin 2,000 IUN** bei yake ilikuwa Sh. 33,000, lakini bei iliyoboreshwa ni 14,900 na huduma ya **Erythropoietin 4,000 IU** ambayo bei ya sasa ni Sh. 66,000 imeboreshwa hadi Sh. 15,500.







## Walioibiwa simu, runinga waitwa polisi kuzitambua

Uk. 3



## Operesheni elimu mlipa kodi



Uk. 2

## Anthony Mavunde kuwajengea watoto

Uk. 3

## Naibu Waziri atoa siku 40 huduma zianze

Uk. 2



# Watu wawili wafariki dunia, 50 wajeruhiwa ajali ya gari

**Na Mwandishi Wetu, Pwani**



WATU wawili wamepoteza maisha akiwemo mtoto wa miezi sita na wengine 50 kujeruhiwa baada ya basi dogo aina ya Tata lililokuwa likitoka Kigogo jijini Dar es Salaam kuelekea Mloka Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani kupinduka na kutumbukia ndani ya mto. Basi hilo lilipitia njia ya Kisarawe.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alifika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe kuwapa pole na kuwajulia hali majeruhi wa ajali hiyo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Kisarawe, alithibitisha vifo vya watu hao na kupokea majeruhi 50 ambao kati yao saba walikimbizwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa matibabu zaidi.

Baadhi ya majeruhi walionusurika katika ajali hiyo akiwemo mama mzazi aliyefiwa na mwanawe, walieleza chanzo cha ajali hiyo kuwa ni mwendo kasi wa dereva.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, pia alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema ilihusisha gari lenye namba za usajili T 275 DRZ iliyokuwa ikitokea Kigogo kwenda Mloka Rufiji.

# Naibu Waziri atoa siku 40 huduma zianze kutolewa

**Na Mwandishi Wetu, Iringa**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tamisemi anayeshughulikia Afya, Dk. Festo Dugange, ametoa siku 40 kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa kukamilisha na kuanza kutoa huduma katika Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) la Kituo cha Afya Mkoga kilichopo Kata ya Isakalilo.

Dugange alitoa maelekezo hayo jana mkoani Iringa katika ziara yake ya kikazi baada ya kutembelea jengo hilo zambalo lilianza ujenzi mwaka 2021, lakini hadi sasa halijakamilika.

Aidha, shughuli za ujenzi zimesimama huku fedha zaidi ya Sh. milioni 130 zikiwa zimetumika kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mbunge na nguvu za wananchi.

"Rais ameleta fedha kwa ajili ya wananchi wa Isakalilo waondokane na umbali wa kupata matibabu kwenda mjini zaidi ya kilomita 17 na umbali huo unasababisha vifo na kinamama wanafariki dunia kwa sababu ya uzembe wa watumishi w manispaa… sasa wekeni kipaumbele hapa ili ifikapo Januari 30, 2024 tunataka wananchi waanze kupata huduma za OPD hapa," alisema Dk. Dugange.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tamisemi, Dk. Festo Dugange

# Chalamila ataka operesheni elimu mlipa kodi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ametaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kufanya operesheni maalum ya elimu kwa mlipa kodi.

Alitoa agizo hilo wakati wa mkutano maalum wa kimkakati na watumishi wa TRA uliofanyika juzi.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila

Alisema kodi ni chanzo cha mapato serikalini hivyo aliwataka mameneja na maafisa wa TRA kwa ujumla wao kufanya kazi zao kwa weledi, kufuata sheria na kutoa elimu kwa umma ili kila mtu ajue umuhimu wa kulipa kodi kwa hiyari bila shuruti yoyote kwa masilahi mapana ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

"Kwa mfano, wanafunzi wa darasa la kwanza mpaka chuo kikuu leo katika Mkoa wa DSM, unapokea si chini ya Sh. bilioni 1.2 kila mwezi kama ada na posho kwa walimu.

"Maana yake TRA tusipokusanya kodi hii kwa mujibu wa sheria watoto hawa hawatapata huduma hizo," alisema.

Aidha aliwahimiza watumishi hao kufuatilia mashine EFD kwa sababu kuna wafanyabiashara wengine huamua wenyewe wazitumie au wasizitumie.

"Hebu mahali popote ambapo hakuna matumizi ya namna hii tuendelee kuwa wakali," alisema.

Aidha alitoa rai kwa wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiyari kwa mujibu wa sheria zilizopo na wasisubirie nguvu ya polisi itumike.

"Uwekezaji unaokwepa kodi haustahili kwenye nchi," alibainisha.

Pia alisema kipindi kijacho ni kipindi cha chaguzi, hivyo, aliwaasa watumishi kuendelea kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria bila kukatishwa tamaa na wanasiasa kwa kuwa kodi ndizo hutumika kufanya maendeleo na kupitia hayo maendeleo ndiyo kura kwa Chama.

Wakati huo huo, Chalamila ameiongeza Kampuni ya Derm Group kwa kuadhimisha miaka 25 ya mafanikio.

Chalamila alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam wakati wa sherehe za miaka 25 ya mafanikio ya kampuni hiyo tangu kuanzishwa kwake.

Akizungumza na watumishi pamoja na wageni waalikwa katika hafla hiyo,

Chalamila alipongeza Bodi na Menejimenti ya Derm Group chini ya uongozi wa Ridhuan Mringo, ambapo alisema kampuni hiyo licha ya kutoa huduma nzuri za kihandisi katika nyanja mbalimbali, imetoa fursa kubwa ya ajira kwa Watanzania.

"Naipongeza Derm Group kwa uwekezaji mkubwa katika Human Capital kwa kuwa ndiyo msingi wa kusonga mbele," alisema Chalamila.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya Derm Group, Mhandisi Mringo, alisema historia imeandikwa kupitia kampuni hiyo ambayo inafanya shughuli mbalimbali za kihandisi hapa nchini ikiwemo ujenzi wa majengo marefu, utengezaji wa vifaa vya umeme na nguzo za zege ambazo kwa sasa hutumiwa na Shirika la Umeme nchini (Tanesco).

# El-Nino yaacha kilio kwa wakulima wa pamba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wa pamba kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa wametaja mvua ya El-Nino inayoendelea kunyesha nchini kuathiri kilimo hicho na kuwasababishia hasara kutokana na mashamba kujaa maji na kuharibu zao hilo linalohitaji mvua ya wastani.

Kwa mujibu wa mtafiti wa zao hilo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Nchini (Tari) Ukiliguru, Dk. Paul Saidia, pamba UKM 08 inayotumiwa na idadi kubwa ya wakulima, inahitaji maji yasiyozidi milimita 500 tofauti na ilivyo kwa sasa maji yameongezeka zaidi.

Wakulima wanataja hali hiyo kushusha uzalishaji wa zao hilo kwa msimu ujao kutokana na mavuno kidogo yatakayopatikana kulinganisha na misimu mingine iliyokuwa na mvua za wastani.

Mkulima wa Kijiji cha Kitwechembogo wilayani Biharamulo, Charles Mbuga, alisema alilima ekari tatu na eneo dogo lililopo kwenye mwinuko, ndilo lililobaki bila kuingiwa na maji ambapo analazimika kusubiri mvua ziishe ili apande upya.

"Matarajio kwa kipindi hiki ni madogo kwani ni tofauti na misimu mingine ambayo tulipata mavuno kutokana na mvua kuwa za wastani na zao hili halihitaji mvua nyingi kama za sasa," alisema mkulima kutoka Kata ya Ruziba.

Mkulima wa kutoka Ibuka, Bundala Maziku, alisema mashamba ya pamba yamejaa maji na sasa wanaendelea kuweka matuta kando ya mashamba ili kuzuia maji kuingia ndani.

# Polisi Dar wanasa mali za wizi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewanasa watuhumiwa wa matukio mbalimbali ya uhalifu.

Miongoni mwa waliotiwa mbaroni, wamo watuhumuiwa wawili wanahisiwa kuendesha Uhalifu wa kutongoza wanawake, kuwalewesha, kuwadhalilisha kingono, kuwapiga picha, kuwatishia maisha na kisha kuwaibia fedha, simu, laptop na vitu vingine vyenye thamani.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam Muliro Jumanne akizungumza jana alisema sambamba na watuhumiwa hao wawili ambao uchunguzi wao unaendelea ili kubaini mtandao wao, watuhumiwa wengine waliokamatwa wamekuwa wakijihusisha na uhalifu wa wizi wa simu za mkononi, laptop, luninga, kamera, subwoofer pamoja na makava ya simu aina mbalimbali.

"Watuhumiwa tuliowakamata watashughulikiwa vikali kwa mujibu wa sheria ili iwe funzo kwa watu wengine wanaodhamiria kuingia kwenye mkumbo wa uhalifu wa aina hiyo" alisema kamanda Muliro.

Katika hatua nyingine kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limejipanga kuimarisha hali ya usalama kwenye maeneo yote ili wananchi waweze kusherehekea kwa amani na utulivu sikukuu za krismasi na mwaka mpya.

# Walioibiwa simu, runinga waitwa polisi kuzitambua




**Na Mwandishi Wetu**

KAMANDA wa Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amewataka wananchi walioibiwa simu na vifaa vingine vya kielektroniki kama vile runinga, kompyuta na redio, kufika Kituo Kikuu cha Polisi kuzitambua mali zao.

Akizungumza na waandishi wa habari kituoni hapo jana, Muliro alisema mali hizo zimekamatwa katika operesheni maalum iliyoanza Septemba, mwaka huu ambapo wamefanikiwa kuwakamata wahalifu 27.

"Watu waje kuzitambua mali zao. Tumekamata kompyuta mpakato 10, simu za mkononi 305, runinga 36, makava ya simu 160, kamera nne na redio tatu (subwoofer)," alisema.

Alisema tayari baadhi ya mali hizo zimeshatambuliwa na hatua za kuwashughulikia wahalifu kwa mujibu wa sheria zinaendelea.

# Wanaokwamisha miradi kukiona

**Na Mwandishi Wetu, Kagera**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mohamed Mchengerwa, amesema wanasiasa na watumishi wa umma wanaokwamisha miradi ya serikali iliyokusudiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwakomboa wakazi wa Bukoba mkoani Kagera, atashughulika nao.

Kadhalika, amesema kama ni madiwani ndiyo wanaohusika, alimweleza Meya wa Halmashauri ya Bukoba kwamba atasimamisha vikao vyote vya Baraza mpaka miradi hiyo ikamalike mara moja.

"Mnatamani mmkwamishe mbunge ili miaka mitano ijayo, aje mwingine, sitakubali jambo hilo, wapo viongozi wa serikali na wanasiasa wanaweka mikono yao kwenye miradi kwa kuweka wakandarasi wao wasiokuwa na viwango," alisema.

Alisisitiza kwamba wakizuia maendeleo kwa kigezo cha kumuangusha kila mbunge anayeongoza eneo hilo, watawanyima haki Watanzania na hilo linasababishwa na viongozi wanaoweka mikono yao.



"Kiongozi yeyote wa serikali anayewajibika Tamisemi, atakayeweka mkono kwenye miradi iliyoletwa na Rais Samia ili isiendelee, sitakubali nataka niwaambie wazi kabisa, wanaofikiria matumbo yao badala ya maendeleo, hilo sitakubali kabisa," alisisitiza.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya Waziri kupokea taarifa kwamba viongozi wa umma na wanasiasa katika Halmashauri ya Bukoba, wanakwamisha miradi ya maendeleo ya serikali.

# Anthony Mavunde kuwajengea nyumba watoto waliofiwa

**Na Mwandishi Wetu,**

MBUNGE wa Jimbo la Dodoma Mjini na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, akishirikiana na Ofisi ya CCM mkoani humo, amejitolea kuwajengea nyumba watoto wawili wa darasa la kwanza ambao mama yao alifariki dunia kwa kudondokewa na nyumba katika Kata ya Mbabala kufuatia mvua kubwa iliyonyesha na kuleta athari kwa nyumba 259 ambazo nyingine zilibomoka na kuezuliwa mapaa.

Hayo yalibainika baada ya Waziri Mavunde kuwatembelea na kuwapa pole wananchi wa Kata ya Mbabala ambao walipata athari ya mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali.

Aidha, Waziri Mavunde alitoa msaada kwa waathirika wa tani mbili za mahindi, magodoro 50, sukari, maharage kilo 200 na maji katoni 100.

Akitoa taarifa ya athari hizo, Mtendaji wa Mtaa wa Nguji, Mbabala Jumanne, alisema Novemba mwishoni na Desemba 5, mwaka huu, mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali ilileta athari kubwa kwa wakazi wa mitaa mitatu ya Kata ya Mbabala na kuwasabishia hasara kubwa ya mali ikiwemo upotevu wa mifugo na kusababisha kifo cha mama Rahel Nguuselo, aliyekuwa amelala na watoto wake wawili.

MAGEUZI MAKUBWA NHIF:

# Rais Dk. Samia ashusha gharama kuchuja damu

**Na Hellen Mwango**

ZAIDI ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Serikali anayoiongoza, kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), imeboresha eneo la huduma za kuchuja damu kwa kupunguza gharama kuanzia Januari, mwakani.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, aliyasema hayo wakati akizungumza na wahariri jijini Dar es Salaam, juzi.

Alizitaja huduma hizo kama Haemodialysis ambayo kwa mujibu wa Mfuko huo bei ya sasa ni Sh. 240,000 wakati bei iliyoboreshwa itakuwa Sh. 200,000.

Huduma nyingine ni Erythropoietin 2,000 IUN ambayo bei yake ilikuwa Sh. 33,000, lakini bei iliyoboreshwa ni 14,900 na huduma ya Erythropoietin 4,000 IU ambayo bei ya sasa ni Sh. 66,000 imeboreshwa hadi Sh. 15,500.

Hata hivyo, akizungumzia huduma za upasuaji, Konga alisema katika kuimarisha upatikanaji wa huduma hizo, NHIF imeboresha gharama za upasuaji unaofanyika mara kwa mara kwa kuongeza gharama za upasuaji kwa hospitali ngazi ya mkoa na wilaya.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kupunguza msongamano wa wagonjwa usio wa lazima katika hospitali za kanda na Taifa, kuwezesha hospitali hizo kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kusogeza huduma karibu na maeneo ya wananchi hivyo kupunguza gharama za kufuata huduma hizo.

Alisema maboresho hayo yanakwenda sambamba na mapitio ya gharama halisi na uchambuzi wa uhalisia wa bei katika soko.

Lakini katika hatua nyingine alisema NHIF imeboresha gharama za upasuaji unaofanyika mara kwa mara kwa kuongeza gharama za upasuaji kwa hospitali ngazi ya mkoa na wilaya ili kupunguza msongamano wa wagonjwa usio wa lazima katika

Hospitali za Kanda na Taifa, kuwezesha hospitali hizo kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kusogeza huduma karibu na maeneo ya wananchi hivyo kupunguza gharama za kufuata huduma hizo. Kuhusu huduma za dawa, alisema maboresho katika eneo hilo yamezingatia mabadiliko katika ngazi za matumizi ya dawa kama ilivyoainishwa mwongozo wa tiba nchini.

"Maboresho yaliyogawanyika katika huduma za dawa ni pamoja na kuongeza jumla ya dawa 124 katika kitita cha mafao cha mfuko kutoka orodha ya Dawa Muhimu ya Taifa (NEMLIT), kuweka mbadala wa dawa 309 katika kitita cha



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

mafao ili kuwianisha na NEMLIT na kuzingatia mabadiliko katika ngazi za matumizi ya dawa," alisema.

Katika kuhakikisha kunakuwa na udhibiti wa matumizi, Mfuko huo unaimarisha utambuzi wa wanufaika katika vituo vya kutolea huduma kwa kutumia alama za vidole, kuweka mfumo (platform) wa kieletroniki itakayowezesha watoa huduma kubadilishana taarifa za mgonjwa miongoni mwa vituo na kuweka utaratibu utakaowezesha wanufaika kuzingatia rufaa.

Aidha, alisema udhibiti mwingine ni kuongeza huduma zitakazohitaji uchangiaji na ukomo wa ugharamiaji kwa baadhi ya huduma na makundi ya wanachama, kuweka mfumo wa utambuzi wa madaktari katika vituo vya kutolea huduma nchini.

Hata hivyo, alisema maoni ya wadau yataendelea kupokelewa na serikali kushauriwa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma bora kwa wanufaika wake.

Baadhi ya maoni ya ujumla kutoka kwa wadau ni kwamba walitaka kuongeza huduma mpya katika kitita cha mafao zinazohusu vifaa pandikizi (implants), huduma za upandikizaji wa viungo (kidney & cholea), huduma za upasuaji wa moyo, huduma za upasuaji kwa njia ya video/mtandao na vifaa bandia (orthosis). Alisema maoni ya wadau yataendelea kupokelewa na Serikali kushauriwa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma bora kwa wanufaika wake.

Alisema utekelezaji wa kitita cha mafao kwa mwaka 2023 utaanza rasmi Januari Mosi, 2024 baada ya machakato kukamilika kwa zoezi la utoaji wa elimu

## Rais Dk. Samia ateua, tengua na kuhamisha

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi, utenguzi na uhamisho wa vituo vya kazi kwa watumishi mbalimbali wa Serikali.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa Mawasilianjo ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, iliyotolewa jana, Rais Dk. Samia amemteua Balozi Meja Jenerali Paul Simuli, kuiwakilisha Tanzania nchini Uganda.

Aidha, amemteua Selwa Hamid, kuwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Igunga akichukua nafasi ya Francis Msabila aliyesimamishwa kazi.

Taarifa ilisema Mariamu Chaurembo, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji Halmshauri ya Mji Tunduma akichukua nafasi ya Lena Nkya, ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Ilisema Fabian Said ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Momba, akichukua nafasi ya Butamo Nuru ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Aidha, amemhamisha kituo cha kazi Dk. Peter Nyanja, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Muleba na kwenda Halmashauri ya Wanging'ombe.

Dk. Nyanja anachukua nafasi ya Maryamu Muhaji ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Manyara.

Pia, Rais Samia amemteua Dk. Khamis Mwinyimvua kuwa Mwenyekiti ya Bodi ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, Dk. Mwinyimvua ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) anachukua nafasi ya Profesa Longinus Rutasitara aliyemaliza muda wake.

# Maafisa ugani kupimwa kulingana na kazi zao

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema mfumo wa kupima utendaji kazi wa maafisa ugani katika Sekta ya Mkonge uko kwenye hatua za mwisho na kwamba kila mwaka kila afisa ugani atapimwa kulingana na kazi alizofanya ikiwamo kuwatembelea wakulima shambani.

Akizungumza katika mkutano wa nne wa wadau wa Sekta ya Mkonge uliofanyika mkoani Tanga hivi karibuni, Bashe aliwataka maofisa ugani kuacha kufanya kazi kwa mazoea na kuwafuata wakulima walipo.

"Tuliwaletea mashine za kupima afya ya udongo, na hivi karibuni tukipata fedha tunanunua magari kwa ajili ya maofisa ugani, tunataka wawe na magari, bado vinakuja vishkwambi, halafu sasa nisikie mtu anabaki ofisini. Lazima atapimwa mtu kutokana na kazi.

"Tunaweka mfumo, sasa ule mfumo unakamilika na lazima watu wajaze ripoti kila siku amemtembelea mkulima gani hata kama umemtembelea hujui tatizo utaweka kwenye mfumo aliyeko wizarani atajua hilo tatizo ni nini," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba alibainisha ongezeko la wakulima wadogo wa mkonge mkoani hapa linatokana na hamasa inayoendelea kutolewa lakini pia ushirikiano mzuri wanaopata kutoka Wizara ya Kilimo.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge (TSB), Saddy Kambona, akizungumzia shamba la Kibaranga ambalo linamilikiwa na bodi hiyo, aliiomba Idara ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuwapatia kanzidata na hati ya shamba hilo.

"Bado kuna mkanganyiko mkubwa kutoka kwa maofisa ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa sababu wao ndiyo walikuwa na ile kanzi data ya wakulima ambao waligawiwa ardhi miaka ya nyuma ambayo tuliiomba waiwasilishe kwetu ili kuepusha migongano lakini hatukuweza kuipata hadi leo.

"Hati ilirudishwa wizarani na ikafutwa kwa hiyo lile shamba halina hati ila lilikuwa limekabidhiwa tu halmashauri kwa agizo la aliyekuwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi na sisi tulivyoliomba kwenye huo mchakato bado halijarudishwa kwetu kwa hati lakini kiutawala linaonekana lipo kwetu," alisema.

Pamoja na mambo mengine, alisema wameanza ukarabati wa korona (mashine ya kuchakata mkonge) ya Kibaranga kwa sababu baada ya kulichukua lile shamba bodi iliwasilisha maombi ya fedha wizarani kwa ajili ya ukarabati wa korona hiyo ambazo walipatiwa na kuanza kufanya mengine yanayolihusu lile shamba.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe

# NEC yamiminiwa sifa Daftari la Wapigakura

**Na Godfrey Sanga**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imepongezwa kwa maandalizi mazuri ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Taarifa iliyotolewa kupitia mtandao wa instagram wa tume hiyo ilisema, pongezi hizo zitolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). Ummy Nderiananga, wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Tume jana jijini Dodoma.

"Hongereni sana kwa kuendesha vizuri zoezi la uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mlilolifanya kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, mwaka huu. Tumeona mmejipanga na mpo tayari kwa uboreshaji," alisema Nderiananga ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye baraza hilo.

Awali, akimkaribisha mgeni rasmi, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Ramadhani Kailima alilijulisha baraza hilo kwamba uboreshaji wa majaribio umefanyika kwa mafanikio.

Kailima alisema katika uboreshaji huo wa majaribio, Tume ilifanikiwa kupima uwezo wa vifaa na teknlojia ya uboreshaji ambalo ndilo lilikuwa lengo kuu la zoezi hilo.

"Tumefanikiwa kupima uwezo wa vifaa na teknolojia japo hatukupata watu waliotumia mfumo wa kujiandikisha kwa njia ya mtandao. Changamoto tumezigundua na tunazifanyia kazi kwa ajili ya maandalizi ya uboreshaji wa daftari," alisema Kailima.

NEC ilifanya uboreshaji wa majaribio kwenye Kata ya Ikoma iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya mkoani Mara na Kata ya Ng'ambo iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora mkoani Tabora kwa siku saba kuanzia Novemba 24 hadi Novemba 30, mwaka huu.



**Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga**

Katika hatua nyingine, Nderiananga aliwaasa wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kushirikiana, kuepuka mambo ya utovu wa nidhamu na kudumisha utamaduni wa kujengeana uwezo wa kiutendaji.

"Mnayo nafasi kubwa katika kuwahamasisha watumishi wenzenu ili waweze kuwa na ufanisi kazini, ufanisi huo utatokana na ushirikiano mzuri kati ya watumishi na viongozi," alisema.

Nderiananga alisisitiza juu ya umuhimu wa kuendelea kuitisha mabaraza ya wafanyakazi kwa kuwa ni jambo la kisheria na linalolenga kuweka mazingira mazuri na ustawi wa wafanyakazi.

## Jela maisha kwa ubakaji

**Na Mwandishi Wetu, Songwe**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Momba, imemhukumu dereva wa bajaj, Ibrahim Salum (35), kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na kosa la ubakaji.

Mshtakiwa Ibrahim alikamatwa Januari 28, mwaka huu maeneo ya Maporomoko mkoani Songwe.

Awali, mshtakiwa alidaiwa kumlaghai mwanafunzi wa darasa la tatu mwenye umri wa miaka tisa kwa kumwambia atamnunulia chipsi kisha akamvutia kwenye nyumba ambayo haijaisha na kutekeleza kitendo hicho.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Momba, Kannonyele alisema Mahakama ilijiridhisha pasipo na shaka ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri na kumtia hatiani mtuhumiwa huyo.

Mshtakiwa alihukumiwa kifungo hicho ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaojihusisha na vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto.

**Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Momba, Kannonyele alisema Mahakama ilijiridhisha pasipo na shaka ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri na kumtia hatiani mtuhumiwa huyo.**



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO


### Kupandisha nauli tofauti na maagizo ya mamlaka



LICHA ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), kutoa tamko la kupanda kwa gharama za usafirishaji (nauli), kwa utaratibu na makadilio maalumu, lakini wapo baadhi ya makondakta wanaozidisha kiwango cha nauli zaidi ya kile kilichopendekezwa na mamlaka husika.

Kufanya hivyo si jambo jema kwani mnaumiza wasafiri (abiria) kwakuwabebesha mzigo mzito tena zaidi ya ule wa awali.

Ninashauri kuacha mara moja vitendo hivyo kwani mkibainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yenu.




## MAONI YA MHARIRI

# Kupunguza gharama za kuchuja damu jambo muhimu kwa wananchi

KATIKA ukurasa wa mbele wa toleo hili, kuna habari inayoelezea hatua ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kuboresha eneo la huduma za kuchuja damu kwa kupunguza gharama kuanzia Januari, mwakani.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, aliyasema hayo wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, juzi.

Alizitaja huduma hizo kama Haemodialysis ambayo kwa mujibu wa Mfuko huo bei ya sasa ni Sh. 240,000 wakati bei iliyoboreshwa itakuwa Sh. 200,000.

Huduma nyingine ni Erythropoietin 2,000 IUN ambayo bei yake ilikuwa Sh. 33,000 lakini bei iliyoboreshwa ni 14,900 na huduma ya Erythropoietin 4,000 IU ambayo bei ya sasa ni Sh. 66,000 imeboreshwa hadi Sh. 15,500.

Hata hivyo, akizungumzia huduma za upasuaji, Konga alisema katika kuimarisha upatikanaji wa huduma hizo, NHIF imeboresha gharama za upasuaji unaofanyika mara kwa mara kwa kuongeza gharama za upasuaji kwa hospitali ngazi ya mkoa na wilaya.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kupunguza msongamano wa wagonjwa usio wa lazima katika hospitali za kanda na Taifa, kuwezesha hospitali hizo kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kusogeza huduma karibu na maeneo ya wananchi hivyo kupunguza gharama za kufuata huduma hizo.

UELEKEO tunachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa hatua hii kwani hakika imezingatia hali halisi ya wananchi wa Tanzania.

Ni ukweli usiopingika kuwa hatua hii itawasaidia Watanzania wengi ambao wanateseka ama kwa kutokana na kipato kidogo ama uwezo kwa ujumla.

Serikali ya Rais Dk. Samia, imedhihisiha kuwa ni sikivu na inayowajali wananchi wake.

Ni matarajio yetu kwamba maboresho hayo yanakwenda sambamba na mapitio ya gharama halisi na uchambuzi wa uhalisia wa bei katika soko.

Tunatoa hongera nyingi kwa serikali na tunaamini kwamba Watanzania wengi wataunga mkono kwa dhati kabisa.

## Wasiliana nasi


| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255753333330 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255787559090 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |




Na Godfrey Sanga
Sangagodfrey26@gmail.com

## JICHO LANGU

# Unaposafiri mwisho wa mwaka zingatia usalama

HUU ni mwisho wa mwaka ambao watu wengi hupendelea kusafiri kwenda kusalimia wazazi wao, ndugu jamaa na marafiki.

Hivyo ni kipindi ambacho watu husafiri sana kwa ajili ya mapumziko ya mwisho wa mwaka.

Kwa wanaokwenda kuwaona wazazi baada ya kutengana nao kwa muda ninawapongeza sana na sisi tunaoamini katika maandiko wanakwenda kuchota baraka nyingi sana kiasi kwamba mimi nawaonea wivu.

Kwa sisi wakazi wa Dar es Salaam, kadiri Krismasi inavyokaribia, tunaona magari yanapungua hata barabarani na hili linathibitisha ukweli kwamba wengi, hususani wenye asili ya Mkoa wa Kilimanjaro wanasafiri sana.

Hata hivyo, ni ukweli pia kwamba safari katika kipindi hiki huambatana na ajali nyingi na hivyo kama unasafiri peke yako au wewe mwenyewe ni jambo la kutulia maanani usalama wako barabarani.

Kutokana na kushamiri kwa ajali mwishoni mwa mwaka, imepelekea watu wengine kuhusisha matukio hayo na imani za kishirikina.

Kuna waodanganyana eti vifo vya mwisho wa mwaka ni tambiko la kuukaribisha mwaka mpya. Hizi ni imani potofu.

Kutokana na imani hizi potofu, imefikia watu wanaogopa na hivyo hawataki kabisa kusikia suala la safariyoyote mwishoni mwa mwaka.

Kimsingi, ajali hutokea kwa sababu ya watu kutozingatia masuala ya usalama bararani. Unakuta mtu hana uzoefu wa kuendesha safari ndefu lakini anataka aendeshe na wengine wanakuwa wanafunzi (learner) katika usukani.

Lakini pia wapo, tena wengi tu ambao huendesha wakiwa wawiliwawili kichwani, yaani wamekunywapombe. Kwa hiyo ni vyema, hata kama unasafiri kwa basi, hakikisha huendeshwi na dereva mlevi au anayeshindana na magari mengine barabarani kwa sababu magari kipindi hiki huongezeka.

Kuna andiko nililiona kwenye magrupu ya Whatsapp, nadhani ni la msingi na la kuzingatia.

Mwandishi wa andiko hilo, akiwalenga zaidi watu wanaosafiri kwa magari yao ameweka takribani mambo 17 ya kuzingatia na mimi nimeonelea kuyaandika hapa.

Mambo hayo ni pamoja kuhakikisha gari yako iko vizuri (imefanyiwa service na wataalamu), penda kusafiri mchana tu, waza kufika salama na si saa ngapi na pia epuka mafuta ya vichochoroni.

Mengine ya kuzingatia, kama unakokwenda ni mbali, yaani km 700 na zaidi basi safari yako unaweza kuikata vipande viwili na pia ukiwa na wasiwasi na uwezo wako wa kuendesha tafuta mtu ukifika mpe posho kidogo na nauli arudi. Hili ni muhimu sana.

Ushauri mwingine kwenye andiko hilo ni kuwa makini sana unapoanza safari na unapokaribia kufika, usipende kusimama porini usipopajua bila sababu au kwa kuchimba dawa na kwamba usiku ukipishana na gari punguza mwendo huku ukiibia kushoto kwako kidogo.

Kuepuka kushindana na gari/mtu ambaye hata hujui anatoka na anakwenda wapi hata kama gari lake ni sawa na la kwako ni ushauri mwingine wa kuzingatia.

Unashauriwa pia kuandaa chakula toka kwako na mtu anayeendesha atumie vyakula vyepesi (bites) zaidi nyama kavu za kutafuna na akili yako (unayeendesha gari) muda wote iwe barabarani na siyo unakokwenda au unakotoka.

Unatakiwa pia kujitahidi njiani si kila mtu ajue unaenda wapi, hakikisha upepo kwenye matairi ya gari uko sahihi kila wakati wote na pia ukumbuke kwamba hiki ni kipindi cha mvua, ukiona inazidi tafuta mahali salama, egesha subiri ipungue kisha uendelee.

La mwisho lakini si kwa umuhimu, hakikisha hakuna gari lolote nyuma linakufuata kwa muda mrefu bila sababu, chukua namba kisha mpishe aende.

# 'Hakikisheni mkulima anapata mbolea bora'

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

WAKAGUZI wa mbolea nchini wametakiwa kufanya kazi yao kwa uadilifu na weledi mkubwa ili kuhakikisha kuwa mkulima anapata mbolea yenye ubora unaokubalika.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Morogoro Dk. Rozalia Rwegasira, alisema hayo mkoani juzi.

Aliwataka wakaguzi hao, kutenda haki wakati wa utekelezaji wa majukumu yao na kuepuka kabisa vishawishi vyovyote vinavyoweza kuwaingiza katika rushwa na hivyo kuleta madhara katika Taifa kwa ujumla.

Jumla ya maafisa kilimo 20 kutoka halmashauri mbalimbali nchini wanahudhuria mafunzo ya siku tatu kuhusu udhibiti wa mbolea ili kuwajengea uwezo kuwa wakaguzi wa mbolea katika maeneo yao.

Alisema katika miaka mitano iliyopita Tanzania imekuwa ikitumia tani 300,000 hadi 600, 000 za mbolea kwa mwaka ambayo ni sawa na asilimia 30 hadi 60 ya lengo ambalo ni tani milioni moja.

Alisema serikali katika msimu wa 2022/23 na 2023/24 imeweka mkakati mahususi wa kuongeza matumizi ya mbolea kwa kutoa ruzuku.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Bwana Allan Mariki alisema mamlaka imejiwekea lengo la kuwa na wakaguzi wawili kwa kila halmashauri ili kuimarisha ufanisi katika udhibiti wa tasnia ya mbolea nchini.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo na kuwapa mbinu sahihi za udhibiti wa ubora wa mbolea kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mbolea Na.9 ya mwaka 2009 na kanuni zake.

Aidha, Mariki amewataka mawakala na wafanyabiashara wa mbolea nchini kutojihusisha na vitendo vya kuchezea mfumo wa mbolea za rukuzu kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao wote watakaobainika kufanya hivyo.



Washiriki wa mafunzo ya wakaguzi wa mbolea wakifuatilia kwa makini mada iliyokuwa ikiwasilishwa na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti Alllan Mariki kuhusu Mamlaka, Majukumu na Maadili ya wakaguzi wa mbolea mkoani Mirogoro.

# Serikali kuboresha huduma bora za afya kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, amewahimiza wabunifu wa huduma za afya za kidigitali kushirikiana na Serikali ili kuboresha huduma bora za kiafya kwa wananchi kupitia TEHAMA.

Dk. Jingu alisema hayo katika Jukwaa la Wabunifu wa Afya ya Kidijitali lililofanyika jijini Dar es Salaam juzi katika Ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere leo lililohudhuriwa na wadau mbalimbali kama vile Mamlaka ya Serikali Mtandao (EGA) na wadau sekta binafsi nchini.

"Tunafahamu kwamba dunia ya sasa ni ya teknolojia na teknolojia za kidigitali. Serikali, kupitia Wizara ya Afya, imeweka mikakati mbalimbali kutumia teknolojia za kisasa katika kuboresha utoaji wa huduma za Afya," alisema.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu

Aidha, Dk. Jingu alisema Serikali, kupitia Wizara ya Afya, imeongeza kasi ya utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi kwa kutumia teknolojia za kidigitali.

Alisema teknolojia hizi zimesaidia kutoa huduma bora kwa haraka, ufanisi, kasi na usahihi zitakazoruhusu upatikanaji wa huduma za afya kwa urahisi.

Alisema Wizara ya Afya imeanzisha Kituo cha Afya cha Kidijitali (CDH) yenye lengo la kuhakikisha wadau wote kwenye sekta ya afya wanafanya kazi kwa pamoja na wanapata njia wanayoweza kushirikiana katika kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya afya ili kuboresha huduma za afya nchini.

"Teknolojia italeta mapinduzi makubwa, na mapinduzi haya yanawezekana, kama tutafanya kazi kwa pamoja," alisema.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona, cheti cha shukrani ya udhamini wa Mkutano wa Nne wa Wadau wa Sekta ya Mkonge uliofanyika Korogwe mkoani Tanga wiki iliyopita. Picha: Mpigapicha Wetu



Waziri wa Uchukuzi wa Tanzania, Profesa Makame Mbarawa

# TPA yasogeza huduma Malawi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imezindua rasmi ofisi yake katika nchini Malawi ikiwa ni hatua ya Mamlaka hiyo kusogeza huduma za Bandari karibu na wateja wake wa nchini humo.

Waziri wa Uchukuzi wa Tanzania, Profesa Makame Mbarawa, alisema, ofisi hiyo itapunguza usumbufu kwa wateja wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka nchini Malawi na watapata huduma zote wakiwa nchini mwao.

Kwa upande wake, Waziri wa Uchukuzi na Ujenzi wa Malawi, Jacob Hara, alisema, ofisi hiyo itakuwa na manufaa makubwa kwa wafanyabiashara wa Malawi na itarahisisha shughuli za usafirishaji wa mizigo kupitia bandari hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, alisema uzinduzi wa ofisi hiyo unatimiza dhamira ya mamlaka hiyo kusogeza huduma kwa wateja wake.

Na Mwalimu Paul Masatu
Simu: +255 766 775 255



# Vitu muhimu vya kuwekeza ndani yako

MAFANIKIO yako hayaanzii nje, yanaanzia ndani yako. Ukitaka kuwa mtu bora na kufanikiwa kwa haraka, ni muhimu sana kuwa na uwekezaji wa kutosha ndani yako. Kwa Lugha nyingine, wewe ulivyo ni matokeo ya uwekezaji ulioufanya ndani yako kwa kukusudia au kwa kutokusudia.

Mwonekano wako wa nje ni taswira ya vile ulivyo ndani yako. Hivyo ni vyema kama utafanya maamuzi leo kujiboresha ndani yako kwanza. Na tunaposema kuwekeza ndani yako tunazungumzia mtazamo wako (Fikra na akili) na moyo wako. Hivyo, ni vizuri pamoja na mambo mengi ukahakikisha kila siku unapata nafasi ya utulivu kusikiliza au kusoma vituvinavyokujenga kama makala hizi zinazoboresha fikra, moyo na mtazamo wako. Leo nataka tutazame mambo muhimu unayotakiwa kuwekeza ndani yako: -

i) Uwezo wako kuona kwa kutumia akili (your mind), hii inaitwa Insight: - Siku zote maisha yako yataelekea uelekeo kule akili yako inakoona, hatua utakazochukua zitategemea unaona nini ndani yako.

Msingi mkubwa ni kuwa huwezi kufanya zaidi ya vile unavyoona. Tambua kuwa, vita kubwa inapiganwa kwenye akili yako, kuamua ni picha gani ikae kwenye akili yako na picha itakayoshinda ndiyo itaamua wapi maisha yako yataelekea.

Kwa hiyo namna moja ya kupigana vita hii ni kwa kuuendeleza huo uwezo wazo wa kuona vizuri yaani kuona sawasawa. Hatima ya maisha yako imebebwa na uwezo wa kuiona hiyo hatima (ability to see your future).

Watu wengi wamewekewa hatma njema sana mbele yao lakini Mazingira ya sasa (circumstances), Mawazo (opinion) za watu, pamoja na hali yako ya zamani ambayo umeiishi (past experiences) yatapambana kutaka kukujengea picha ya udhaifu kwenye akili yako, hakikisha unapambana kukataa picha hizo zisikae kwako na kujiona duni. Kwa sababu picha unayoioina ndiyo itakayotawala maisha yako. Pambana kufuta picha za ajabu hata kama Unahisi ni uhalisia wa sasa, hakikisha unaona kule unakotaka kwenda. Siku zote hakikisha picha ndani yako inakuonesha wewe ni mwenye mafanikio, hakikisha unaona ndoto yako ikitimia, hakikisha unauona mwisho mwema kwenye akili yako (Begin with the end in mind).

ii) Jambo la pili ni uwezo wako wa kulipa gharama: - Ili ndoto hiyo njema unayoiona kwenye akili yako itimie, ili mwisho huo unaouona kwenye akili yako utimie, kuna mambo unatakiwa uyafanye, kuna hatua unatakiwa uchukue na lazima kuwepo utekelezaji. Hapa tunazungumzia bidii kubwa na kulazimisha matokeo. Jambo hili si rahisi, ni uwezo wa kufanya kile unachopaswa kufanya (hata kama hujisikii kufanya) "Self-discipline"

Kulipa gharama ni kuhakikisha una uwezo wa kusimamia na kutekeleza kauli zako (To walk the talk) wakati wengine wanaita "Integrity". Kuna watu wana malengo mazuri, lakini wanakosa nidhamu na uwezo wa kuchukua hatua ili malengo yao yatimie. Uwezo huu unaweza kuendelezwa ndani yako, zoezi hilo ni sehemu ya mchakato wa ukuaji wako binafsi (personal development).

iii) Jambo la tatu ni uwezo wako wa kuchukua hatua: - Muujiza wowote ule ili uwe muujiza, lazima utanguliwe na kuchukua hatua, kwa maneno mengine kuchukua hatua ni sehemu ya muujiza au mafanikio ya ndoto yako. Hata ukitamkiwa unabii, ukipokea mahubiri au mafundisho, tambua kuwa, athari chanya za huo unabii/ mafundisho/mahubiri lazima ziguse kwanza namna yako ya utendaji kwa maana ya kuchukua hatua.

Unabii/mafundisho/mahubiri yasiyo na mchango katika kuboresha namna yako ya kuchukua hatua, ni nadra sana kukuletea muujiza, lazima uwe na uwezo wa kuchukua hatua pale ambapo ulikuwa huwezi kuchukua hatua, au kukuongezea ufanisi katika namna yako ya kufanya mambo.

Ukitaka kuona mafanikio, chukua hatua (take actions), fanya mambo kwa bidii na ongeza ufanisi (ubora) katika utendaji wako. Wakati wengi wetu tunajiandaa kwenda kwenye "Crossover night" kutolewa matamko ya mwaka mpya, kumbuka hili, unataka kuona muujiza kwenye maisha yako kwa mwaka mpya wa 2024? Utendaji kwa maana ya kuchukua hatua ni sehemu ya muujiza. Bila kufanya hivyo, hakuna mafanikio. Fanya zaidi,

Boresha ulichokuwa ukifanya awali na fanya tofauti na ulivyokuwa mwanzo.

Ukifanya haya na mengine yaliyo bora, utaona muujiza wa mafanikio.

Wework Consult
Your Partner in Growth

# Waziri: Dawasa shirikisheni wananchi kujua bili za maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewataka wasoma mita wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Dawasa), kuhakikisha kwamba wanashirikisha wananchi kwa ukaribu kujua kiwango cha maji walichotumia ili wajue bili wanayopaswa kulipa.

Waziri Aweso alitoa agizo hilo wakati wa hafla ya kusaini makubaliano ya utekelezaji wa miradi ya maji kati ya Dawasa na Kampuni ya Shanxi Kibaha Mkoa wa Pwani mwishoni mwa wiki.

Miradi hiyo ina thamani ya Sh. bilioni 48 na kukamilika kwake kunatarajiwa kuimarisha uchumi wa viwanda katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kutokana na uhakika wa upatikanaji wa majisafi kwenye maeneo ya viwanda.

Waziri aliitaka Dawasa kuhakikisha inasimamia vyema utekelezaji wa miradi ya maji Pangani, Kimbiji mpaka Chuo cha Uhasibu na Kwala kwa ufanisi ili iweze kuwa na tija kwa wananchi na kukuza uchumi wa viwanda kwa Mkoa wa Kibaha.

Aweso alisema miradi hiyo ni tegemeo kubwa kwa wakazi wote pamoja na kukuza maendeleo ya Mkoa wa Pwani na maeneo ya Dar es Salaam, hivyo mkandarasi anatakiwa asimamiwe kwa ukaribu ili tija ya mradi ionekane kwa wananchi.

Waziri Aweso alieleza kuwa miradi hiyo ikikamilika kusiwe na usumbufu katika kuunganisha wananchi kwenye huduma kwa kuwa ni haki ya kila mmoja kupata huduma ya majisafi kwa wakati na aliwataka wananchi nao watimize wajibu wao kwa kulipa bili kwa wakati.

Waziri Aweso aliitaka Dawasa kuendana na mabadiliko ya teknolojia kwa kuanza kutumia mita za malipo ya kabla (prepaid meters) ambazo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa malalamiko ya bili za maji.

"Huu ni wakati sahihi kwa Wizara ya Maji kuanza kutumia teknolojia hii ya mita za kulipa kabla kwa kuwa zitasaidia kuleta mageuzi nchini kwenye utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi," alisema Aweso.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, alisema kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya majisafi Pwani, upatikanaji wa maji kwa Mkoa wa Pwani umefikia wastani wa asilimia 86 na juhudi zinaendelea za kuboresha huduma.

"Tunaridhishwa na jitihada za Dawasa uboreshaji wa huduma na tuna imani kwa kasi hii tutaweza kufikia asilimia 95 ya upatikanaji wa huduma kwa mwaka 2025," alisema Kunenge.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Kiula Kingu alisema jumla ya miradi mitatu ikiwemo mradi wa Kwala, Pangani na mradi wa Kimbiji mpaka Chuo cha Uhasibu imesainiwa kwa lengo la kuboresha huduma kwa Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam.

Alisema miradi hiyo inatekelezwa kwa fedha za Serikali na Dawasa kwa Sh. bilioni 48, ambapo mradi wa maji Pangani utanufaisha wananchi 14,868 wa maeneo ya Kibaha - Msufini, Lulanzi, Tamco na Pangani.

Mradi wa maji Kimbiji mpaka Chuo cha Uhasibu, unalenga kunufaisha wakazi wa Tazara, Ukonga mpaka Gongo la Mboto. Pamoja na mradi wa Kwala unaolenga kunufaisha wananchi 7,901 wa Bandari Kavu pamoja na vitongoji vya Kwala.



**Mkuu wa wilaya Kigoma, Salum Kali (kulia), akikabidhi zawadi kwa mmoja wa wazee wanaoishi kwenye kituo cha wazee wasiojiweza Silabu, Manispaa ya Kigoma Ujiji. Picha: (Mpigapicha Wetu.)**

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Desemba 20 - 26, 2023 |

KOLAMU

TEKNOLOJIA

JAMII

# Serikali ipongezwe, si kunyooshewa kidole

UK. 12 & 13



Jamii

# Serikali inavyomwaga mabilioni kufungua mkoa mpya wa Songwe

**Na Lauden Mwambona, Songwe**

SONGWE ni mkoa wa mwisho kuundwa hapa nchini kati ya mikoa yote ya Tanzania bara na visiwani. Mkoa huu uliundwa mwaka 2016 kwa kumega sehemu ya ardhi ya Mkoa wa Mbeya ili kusogeza huduma mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiuchumi karibu na wananchi.

Maeneo ya mkoa wa Mbeya yaliyounda Mkoa wa Songwe ni wilaya za Ileje na Mbozi, wakati Wilaya ya Chunya imekatwa kipande.

Mkoa wa Songwe kwa sasa una wilaya za Ileje, Mbozi, Momba ambayo eneo lake limetoka kwenye eneo la Mbozi na Wilaya ya Songwe ambayo eneo lake lilikuwa sehemu ya Wilaya ya Chunya.

Mkoa huu una halmashauri tano ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Halmashashauri ya Wilaya ya Songwe, Halmashauri ya Wilaya ya Momba na Halmashauri ya Mji wa Tunduma ambayo imo ndani ya Wilaya ya Momba.

Makao makuu ya Mkoa wa Songwe yako Wilaya ya Mbozi katika Mji wa Vwawa.

Kutokana na upya wake, Mkoa wa Songwe ulianza kwa kukutana na changamoto mbalimbali zikiwamo za utoaji wa huduma za afya, elimu, maji, na barabara.

Mtandao wa barabara ambao makala haya yanauangazia kwa kina zaidi, unatajwa kwamba ilikuwa ni moja ya kero kubwa katika kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji mkoani humo.

Mtandao wa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA) mkoani Songwe una urefu wa kilometa 3,341.63 ambazo zinaunganisha tarafa, kata, vijiji na vitongoji.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Suleiman Bishanga anasema zaidi ya kilometa 1,073.32 ya barabara kuu zinazounganisha Songwe na mikoa au nchi jirani zinasimamiwa na Tanroads.

Barabara hizo ni pamoja barabara inayotoka Mbeya kwenda Zambia na barabara za mikoa ambazo nyingi bado hazina lami.

Kati ya Novemba 23 hadi Novemba 25, 2023, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alifanya ziara katika mkoa huu mpya ambapo alizindua, aliweka mawe ya msingi na kukagua miradi mbalimbali ikiwamo ya elimu, afya, maji na barabara.

Pamoja na mambo mengine, Waziri Mkuu aliwaambia wakazi wa mkoa wa Songwe kwamba pamoja na kuwatembelea, alikuwa amebeba salaamu za Rais Samia Suluhu Hassan kwao.

Ujio wa kiongozi huyo ilikuwa faraja kwa wakazi wa Mkoa wa Songwe ambao, mbali na sasa kupata huduma kwa karibu kulinganisha na wakati mkoa ulipokuwa haujaanzishwa, wanaanza pia kuona manufaa ya kuundwa kwa mkoa huo kutokana na huduma mbalimbali kuimarika.

Waziri Mkuu aliwaambia Wanasongwe kwamba Rais Samia anatambua umuhimu wa kuujenga mkoa huo mpya katika sekta zote na hivyo akawasihi wananchi kuendelea kuiamini na kuiunga mkono serikali yao.

Anasema katika kipindi cha mwaka 2023/24 pekee, Serikali ya Rais Samia imemwaga zaidi ya Sh bilioni 579 kwa ajili ya mkoa wa Songwe kupitia halmashauri zote.

Majaliwa alisema hayo wakati akiwahutubia wananchi wa Wilaya ya Mbozi waliofika eneo ambalo Waziri Mkuu huyo alikagua ujenzi wa barabara ya lami kutoka Ruanda kupitia Nyimbili-Hasamba hadi Ileje.

Anasema Serikali imeweka kipaumbele cha ujenzi wa barabara za mpakani mwa Tanzania na nchi jirani ambazo ni za kimkakati.

Anasema barabara hizo ni pamoja na ya kuanzia Bahari ya Hindi mkoani Mtwara, mpakani mwa Tanzania na Msumbiji hadi Ruvuma, eneo la Mbambabay kwenye Ziwa Nyasa, Mpakani mwa Tanzania na Malawi.

Anasema kwenye Ziwa Nyasa Serikali imeboresha usafiri wa meli kwa ajili ya abiria na mizigo hadi bandari ya Itungi iliyoko Kyela mkoani Mbeya na ambayo pia inapakana na Malawi kupitia Ziwa hilo la Nyasa.

Anasema kutoka Bandari ya Itungi, Serikali inajenga barabara ya lami hadi Kasumulu wilayani Kyela ikiwa na lengo na kuunganisha bandari hiyo na barabara ya Ileje kuanzia Kasumulu hadi Msongole-Tunduma-Sumbawaga-Katavi na kuendelea Kigoma hadi Biharamulo mkoani Kagera.

Barabara hizo anasema zitawarahishia usafiri wananchi na nchi jirani za Msumbiji, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Rwanda.

Waziri Mkuu anasema Serikali pia inatambua kwamba mkoa wa Songwe ni mkoa wa kimkakati kiuchumi kwani unapitisha mizigo mingi, hivyo barabara ya kuanzia Igawa Mkoani Mbeya hadi Tunduma itaboreshwa.

Hoja hiyo inafafanuliwa pia na Kaimu Meneja wa Tanroads, Mhandisi Suleiman Bishanga ambaye anasema Serikali ya Rais Samia kupitia Wizara ya Ujenzi imepanga kuanza ujenzi wa barabara za lami katika maeneo zaidi ya manne mkoani humo.

Bishanga anasema serikali inatarajia kuanza ujenzi wa barabara ya lami kuanzia Isongole hadi Isoko ikiwa ni moja ya mkakati wa kujenga barabara ya lami hadi Kasumulu wilayani Kyela.

Aidha anasema pia upo mradi wa kujenga barabara ya kilometa karibu 30 kwenye barabara ya kwenda Mji wa Mkwajuni wilayani Songwe ikianzia Mbalizi wilayani Mbeya.

Anasema serikali pia inatarajia kuanza ujenzi wa kilometa 50 za lami katika barabara inayoanzia Mlowo Mbozi kuelekea Kamsamba ambako kuna uzalishaji mkubwa wa mazao.

Aidha anasema serikali pia inajenga kipande cha barabara kuanzia Ruanda hadi Idiwili chenye urefu wa kilometa 21 katika barabara yenye urefu wa kilometa 79.69 hadi Itumba wilayani Ileje.

Anasema kwa kuanzia, tayari mkandarasi ameanza kujenga kilometa mbili za lami.

Ujenzi wa barabara hiyo anasema utakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya kuanzia Mahenje kupitia Hasamba hadi Mji wa Vwawa, Mbozi.

Kwa mujibu wa Bishanga barabara zinazojengwa zitakuwa na taa za barabarani maeneo ya watu, mijini na vijiji

Anasema serikali pia imetoa fedha kwa ajili ya usanifu wa barabara muhimu ikiwamo inayounganisha wilaya za Ileje na Rungwe ya kuanzia Kyimo Kijiji Kitulivu (maarufu KK) kupitia Ikuti -Luswisi- hadi Itumba.

Barabara nyingine zilizo katika mpango wa kujengwa ni za kutoka Itumba -Ibaba - Shingamba mpaka Mbalizi.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kaskenya, akiwa kwenye msafara wa Waziri Mkuu, anasema Rais Samia amepania kuigungua Tanzania kwa kuboresha miundombinu ya barabara.

Mhandisi Kasekenya anasema kwa mara ya kwanza Watanzania watashuhudia ujenzi wa kilometa zaidi ya 2,000 za barabara za lami maeneo mbalimbali nchini.

Anasema barabara hizo zitajengwa kwa mpigo, kwani wakandarasi walishasaini mikataba na kinachosubiriwa ni kuanza kazi.

Kasekenya anatoa wito kwa Watanzania kutoa ushirikiano maeneo yote ambako barabara zinajengwa ili kazi ifanyike badala ya kuweka migogoro.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael anamshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za miradi mbalimbali ya barabara na kwamba kwa sasa takribani barabara zote za changarawe zinazosimamiwa na Tanroads na zile za Tarura zinapitika wakati wote.





Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Hata huku watunzi wa riwaya wanapuuzwa!

ALIPOSOMA makala iliyozungumzia namna watunzi wa riwaya wa Tanzania wanavyobaki na visa vyao vizuri kwenye vitabu huku watayarishaji wa filamu nchini wakihangaika na visa vya hovyo au kuiba mawazo ya wengine, akaguswa na kunipigia simu.

Huyu alikuwa mtu wa pili kuguswa na makala hiyo niliyolenga kuwasaidia watayarishaji wa filamu nchini kujua mahala wanapoweza kupata hadithi zenye mikasa ya kuvutia kipindi hiki wanapotakiwa kuandaa filamu na kisha 'kuziuza' Azam, kituo ambacho kimetangaza kuanza kuzipokea Januari mwaka kesho.

Itakumbukwa msomaji mwingine ambaye pia ni gwiji la usomaji wa riwaya nchini, Peter Chapusa, aliniambia baada ya kusoma makala hiyo kwamba wezi wa kazi za waandishi wa riwaya si watengeneza filamu pekee, bali pia waandishi wa riwaya. Nilijadili hoja zake katika makala iliyopita.

Huyu wa pili ambaye hakuniruhusu kutaja jina lake gazetini, alijitambulisha kwamba ni mzoefu wa tasnia ya filamu nchini na aliponitajia jina lake nikalikumbuka.

Alianza kwa kukubaliana na mimi kwa asilimia 100 kwamba watengeneza filamu wengi si watunzi wa visa motomoto lakini wamelala usingizi kwa kutojua vitabu vinaweza kuwafikisha mbali.

Akaniambia kwamba, makala ile imemfungua sana macho yeye na kundi lake. Akasema moja ya filamu ya Tanzania inayofanya vizuri ndani na nje ya nchi kwa sasa, ikizoa tuzo za kimataifa lukuki, ni ya 'Vuta N'kuvute' (Tag of War) iliyotokana na kitabu cha mtunzi galacha na mtu aliyezoa tuzo kadhaa katika fasihi andishi nchini, Shafi Adam Shafi. Filamu hiyo imetayarishwa na Amir Shivji.

Kisha huyo bwana akaniambia kitu ambacho ndicho hasa sababu ya kuandika makala haya. Kwamba katika tuzo zinazosimamiwa na Bodi ya Filamu Tanzania zilizotolewa Jumamosi iliyopita (16 Desemba, 2023), kati ya vipengele 34 vilivyoshindanishwa hakuna kipengele cha mtunzi au tuseme mwandishi bora wa kisa kilichotumika kwenye filamu, makala au mchezo wa kuigiza!

Kwa kiasi fulani sikuamini, nikaamua kusubiria Jumamosi ya tuzo ili nihakikishe. Naam, Jumaosi ikafika. Kwa kuwa sikualikwa (nani ananijua huko?), nikakaa mbele ya runinga, sebuleni kwangu kufuatilia. Na kweli katika vipengele hivyo 34 sikusikia kilichomhusu mwandishi wa hadithi iliyotumika kutoa filamu ndefu, filamu fupi, makala na kadhalika. Wewe kama ulifuatilia, ulisikia?

Katika hafla hiyo, Bodi ya Filamu pia ilitoa tuzo maalumu kwa viongozi na kisha kwa watu watano ambao wamefanya makubwa katika tasnia ya filamu nchini. Halikadhalika, watu kadhaa akiwemo Mama Tecla Mjata walizungumziwa na watu maalumu walioandaliwa kutokana na mchango wao katika tasnia. Katika kundi hili hakukuwa pia na jina la mwandishi!



Unaweza kudhani kwamba labda ni kwa kuwa filamu zilizozoa tuzo usiku huo zikiwemo tuzo maalumu pengine hakuna inayotokana na kitabu kinachofahamika, ingawa ninachofahamu mimi kila filamu yenye sifa ya kuitwa filamu lazima iwe na mwandishi wa hadithi na mwandishi wa mwongozo (script).

Lakini, kati ya watu waliopewa tuzo kwa mchango wao katika tasnia ya filamu ni Amir Shivji na filamu yake ya Vuta N'kuvute. Pamoja na Msemaji wa Bodi kueleza namna filamu hiyo ilivyofanya vizuri kimataifa na ndio maana akapata tuzo maalumu, jina la mtunzi ambaye nina hakika hakualikwa pia kwenye hafla hiyo, Mzee Shafi, halikutajwa kabisa. Ninarudia tena, halikutajwa kabisa. Halikutajwa hata kwa bahati mbaya!

Hii mimi imenipa picha kwamba hata Bodi yetu ya Filamu haijui umuhimu wa waandishi wa visa vinavyofanya filamu nzuri. Haijui ni wapi filamu nzuri zinaanzia kama tunataka kufika mbali kama inavyochanja mbuga filamu ya Vuta N'kuvute. Bodi haijui kwamba hata filamu nyingi za Hollywood zinatokana na vitabu. Haijui!

Katibu Mtendaji wa Bodi hiyo na washereheshaji wa hafla hiyo, walitaja makundi ya watu walioalikwa kwenye hafla hiyo kama Baraza la Sanaa (BASATA), Baraza la Kiswahili (BAKITA) na makundi mengine.

Lakini asubuhi yake, nilimuuliza mmoja wa viongozi wa Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira (UWARIDI), Maundu Mwingizi, kama umoja huo ambao ndio mashuhuri zaidi nchini kwa waandishi bunifu kama walipata mwaliko, akasema hawakupata!

Nikakumbuka andiko lake huyohuyo, Maundu, ambaye alishangaa sana kuona makundi ya watu mbalimbali yakialikwa wakati wa uzinduzi wa Ikulu ya Chamwino, Dodoma, lakini watunzi wa riwaya na mashairi hawakualikwa!

Katika andiko lake ambalo lilikuwa na kichwa cha habari 'Tukisahaulika sasa tutakumbukwa lini?' Maundu alianza kwa kuelezea hafla ya kumwapisha Rais wa 46 wa Marekani, Joe Biden, Januari 2021, ambapo mbali na wasanii wakubwa duniani kuhudhuria, pia alialikwa msichana mdogo wa miaka 22, Amanda Gorman ambaye ni mtunzi wa mashairi.

Maundu anasema mbali na kualikwa pia alipatiwa fursa ya kusoma shairi lake liitwalo The Hill we Climb, fursa ambayo, ndani ya siku moja tu ilisababisha vitabu vyake viwili; Change Sings: Children Anthem na cha The Hill we Climb, kupanda chati na kushika nafasi mbili za juu kimauzo kwenye orodha ya Amazon.

"Fauka ya hayo, ndani ya siku hiyohiyo moja, mamilioni ya wafuasi (followers) walifurika katika kurasa zake za mitandao ya kijamii," aliandika Maundu mwenye vitabu kadhaa kikiwemo cha Fumbo, ambacho siku kikitengenezwa filamu mtaniamba!

Kisha Maundu akaandika maneno haya ambayo Bodi ya Filamu na taasisi nyingine za kiserikali zinapaswa kuyafanyia kazi: "Kutokana na tukio hilo, Ikulu ya White House ilipeleka ujumbe duniani, namna inavyothamini hadhi na kukuza vipaji vya watunzi wao wa vitabu, sanjari na juhudi zake katika kuhamasisha usomaji wa vitabu, kitu ambacho kinachochea maarifa katika bongo za watu wake, na kusisimua ubunifu katika ukuaji wa vipawa vyao. Tuulizane: ni akina 'Amanda' wangapi nchini mwetu wanaofisha ubunifu wao na kuzika vipaji vyao kwa kukosa hamasa kutoka katika majukwaa makubwa ya wenye mamlaka?"

Maundu akazidi kuandika: "Lakini, anapoalikwa Ommy Dimpoz, akasahulika mzee Shafi Adam Shafi (wa Kuli, Kasri ya Mwinyifuadi, Mbali na Nyumbani, Vuta N'kuvute nk) huko ni kupuuzwa; anapoalikwa Christian Bella, akasahulika Hussein Tuwa (wa Mfadhili, Mkimbizi, Mdunguaji, Bondia nk) huko ni kupuuzwa; anapoalikwa Steve Nyerere, akasahulika Prof. Emanuel Mbogo (wa Watoto wa Mama Ntilie, Malkia Sitti bint Saad, nk) huko ni kupuuzwa; anapoalikwa Hajji Manara, akasahulika Richard Mabala (wa Hawa The Bus Driver, Mabala The Famer, nk), huko ni kupuuzwa.

"Sasa kwa nini tunawapuuza au tunawasahau watu ambao kupitia kalamu zao wanalinda tamaduni zetu na kuchochea maarifa yetu? Umeshajiuliza ni kwa nini, wanenguaji na hata machawa wa wasanii wanaalikwa Bungeni halafu washindi wa tuzo za uandishi wa vitabu (riwaya, mashairi) za Safal-Cornell na Mwalimu Nyerere, wanasahaulika? Ni kupuuzwa tu," akaandika Maundu.

Tusimame hapo nijipigie debe kidogo: Mimi, mwandishi wa makala haya, ndiye Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu upande wa riwaya lakini sijawahi kualikwa kokote!

Turudi kwa maneno kuntu ya Maundu alipozidi kuandika haya: "Katika hali kama hiyo, unadhani kijana aliyewasoma akina Richard Mabala, Hussein Tuwa, kisha akaishia kuwaona tu Facebook na Twitter, anapokuja kuwaona Ommy Dimpoz na Steve Nyerere wakiwa na Rais wa nchi kwenye hafla kubwa za kiserikali, atatamani kuja kuwa nani baadaye kati ya mwanamuziki na mwandishi? Atapenda kusoma vitabu au kusikiliza nyimbo? Sisemi kwamba hatuhitaji wanamuziki, waigizaji, nk, la hasha. Bali tunahitaji mchanyato wa wanasanaa na wanataaluma toka katika nyanja mbalimbali."

Maundu angeweza pia kusema kwamba mamlaka husika zinaweza kuwaacha waandishi wa riwaya wote, lakini angalau zikaalika mabinti wawili, Laura Pettie na Lilian Mbaga ambao wamejitokeza kuwa mahiri katika uandishi wa riwaya ili kuvuta wasichana na wanawake kuingia katika fani.

Nihitimishe kwa nukuu hii kutoka kwa Maundu inayofaa kuandikwa kwa wino wa dhahabu: "Watunzi wa vitabu (riwaya, mashairi, nk) wanazo kofia mbili vichwani mwao; moja, ni wanataaluma. Hii ni kwa sababu vitabu vyao vinaandikwa kitaaluma na vinatumika katika shughuli za kitaaluma; pili, ni wana sanaa, kwa sababu vitabu vyao (riwaya, ushairi, nk), kama ilivyo kwa nyimbo na uigizaji, ni tanzu za fasihi. Na fasihi ni tanzu ya sanaa. Kwa hivyo, washairi na wanariwaya ni wasanii pia. Je, unayajua madhara ya kumsahau mtu ambaye asipoigusa jamii kitaaluma, ataigusa kisanaa?"

Tafuta mjibu.

*NB: Usisahau kusoma kitabu cha Sihusiki kiganjani mwako kupitia hii link: https://www.tupohapa.com/hkibari/*

Jamii

## UHAMAJI WA HIARI NGORONGORO:

# Serikali ipongezwe, si kunyooshewa kidole



MAKAZI MAPYA

**Na Hamisi Kibari**

HIVI karibuni, Serikali ya Tanzania ililazamika kutoa ufafanuzi kuhusu hatua ya kuwahamisha Watanzania wenzetu wanaoishi katika Hifadhi ya Ngorongoro ikisema haitumii nguvu bali inawaondoa kwa hiari ili kuilinda hifadhi hiyo.

Ufafanuzi huo ulitolewa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, kufuatia kile ambacho, kwa mujibu wa taarifa za mitandao, Bunge la Umoja wa Ulaya (EU), lilishauri kufanyike uchunguzi huru ili kuangalia namna ya kushughulikia sakata hilo pasi na uvunjifu wa haki za binadamu.

Ilikuwa ni tarehe 14 Desemba, 2023, taarifa zinaonesha kwamba Bunge la EU lilipitisha azimio la kuiomba Serikali ya Tanzania, kuruhusu waangalizi wa EU kutembelea katika maeneo yenye mgogoro.

Vilevile, bunge hilo likaiomba Serikali ya Tanzania, kuketi mezani na wananchi jamii ya Wamasai ili kuangalia namna bora ya kumaliza mzozo huo.

Katika majibu yake, Msemaji huyo wa Serikali amekaririwa akisema: “Serikali inaendelea kusisitiza kwamba, zoezi hili ni la hiari. Wananchi waepukane na taarifa potofu kuwa kuna uvunjwaji wa haki za binadamu au uondoaji wa watu kwa kutumia nguvu. Moja ya sababu za kuwahamisha ni usalama wa wananchi na kulinda eneo la Ngorongoro ili libaki salama.”

Matinyi anasema Serikali iliamua kuchukua uamuzi wa kuwaondoa kwa hiari wananchi hao wa jamii ya Kimasai, Wahadzabe na Wadatoga (si Wamasai pekee kama inavyodhaniwa na wengi) ili kudhibiti ongezeko la idadi ya watu na mifugo, inayoelezwa kuhatarisha uwepo wa hifadhi hiyo.

Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba idadi ya watu imeongezeka kutoka 8,000 wakati hifadhi hiyo inaanzishwa mwaka 1959 hadi kufikia watu 115,000 (kutoka kaya zaidi ya 22,000) na mifugo takribani 800,000.

Kwa mujibu wa machapisho mbalimbali kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco), eneo hili linapaswa kukaliwa na watu wasiozidi 25,000 na idadi ya malisho ya mifugo pamoja na wanyamapori isiyozidi 254,000. Lakini tayari mifugo pekee ni 800,000!

### UTOAJI ELIMU

Serikali kabla ya kuanza kutoa ruhusa wananchi hao kuhama kwa hiari, ilianza kwa kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuihifadhi Ngorongoro, hasara wanazopata wananchi kwa kuendelea kuishi Ngorongoro huku wakiongezeka ikiwemo usalama dhidi ya wanyama wakali na faida za kuhama itakazopata hifadhi na wananchi wenyewe.

Taarifa zinaonesha kwamba kwa sasa wananchi wengi wameshaelewa umuhimu wa kuiacha hifadhi na wanajua kwa kuendelea kubaki hifadhini, wanakosa huduma za msingi ambazo wenzao wa maeneo mengine, wanazipata. Pia wanajua kwamba yeyote anayeamua kubaki hifadhini, ameamua pia kuendelea kubaki masikini, yeye na familia yake!

Uelewa huu ndiyo umekuwa ukisababisha makundi kwa makundi ya watu kujiandikisha kwa wingi ili kuondoka Ngorongoro.

Mzee wa kimila, Laigwanani Naftali Mollel, kutoka Kata ya Endulen, aliwahi kunukuliwa na



MAKAZI YA NGORONGORO

Jamii



vyombo vya habari akisema:

"Tumehamasika na kuamua kujiandikisha kwa wingi ili tuipishe hifadhi iendelee kutuingizia mapato, wanyama wamekuwa wengi na watalii wamekuwa wengi, tunaomba wote ambao wanatamani kuondoka, wafanye maamuzi, wakati ni sasa na Serikali ya Awamu ya Sita ipo tayari kuwasaidia."

**SERIKALI KUTENGA MAENEO**

Kuhusu zoezi la kuwaondoa wananchi, Matinyi anasema serikali imetenga maeneo maalumu kwa ajili ya watu wanaotaka kuhamia kwa hiari, ambapo wanahamishwa bure pamoja na kulipwa fidia.

Anasema maeneo hayo wanakohamishiwa, yamewekewa miundombinu ya ufugaji pamoja na huduma nyingine za kijamii.

Kabla ya zoezi zima, taarifa zilizopo zinaonesha kwamba Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, ilitangulia eneo wanakohamishiwa wananchi hao, Msomera na kuweka mipaka inayosaidia kuonesha matumizi bora ya ardhi.

Kuonesha serikali ilivyo makini, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mkababu kilichopo katika Kijiji cha Msomera, Yohanna Mapashi, aliwahi kukaririwa akisema kwamba zoezi la upimaji ardhi, lilitatua changamoto za migogoro ya ardhi baina ya wenyeji na wageni waliohamia kijijini hapo kutoka Hifadhi ya Ngorongoro kwani wenyeji walikuwa na hofu ya kupoteza maeneo yao, jambo ambalo lilijibiwa vyema na serikali.

"Tulikuwa tunadhani tumesahaulika na serikali, watu walikuwa na hofu ya kuchukuliwa maeneo yao sababu tulikuwa ni kama tumevamia japo tumeishi kwa muda mrefu huku (Msomera), sasa tunapoona Serikali imetukumbuka na sisi tunapimiwa na kugawiwa maeneo kwa kweli tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita na tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutuletea wataalamu," anasema Mapashi.

Ikumbukwe kwamba Kijiji cha Msomera kilianzishwa ndani ya lililokuwa Pori Tengefu la Handeni lililovamiwa na wananchi na kuanzisha kijiji hicho. Hata hivyo, Serikali iliamua kufuta pori hilo, ambapo kwa sasa linakaliwa na wenyeji wa kijiji hicho na wageni wanaohamia kwa hiari yao kutoka kwenye Hifadhi ya Ngorongoro. Wapo wanaochelewa kuhama siku wakipata 'akili' watakuta aridhi hiyo tengefu imejaa.

**FAIDA LUKUKI**

Mbali na kujengewa nyumba za kisasa, kuhamishwa bure na kulipwa fidia, serikali imejenga bwawa kubwa la kisasa ili kunyweshea maji mifugo.

Kila kaya pia inapatiwa ekari 2.5 mpaka tatu katika eneo analopewa mtu lenye nyumba ya kisasa yenye vyumba vitatu huku ikiwa na hati. Kwa hiyo mtu anaweza kutumia hati hiyo kuombea mikopo.

Lakini kila mtu amepewa wastani wa eneo la ekari tano kwa ajili ya malisho. Pia kuna eneo la wazi ambalo mtu yeyote anaweza kulisha mifugo yake.

**KIFUNGO BARIDI**

Binafsi, ninalifananisha eneo la Ngorongoro na gereza baridi kutokana na sheria zilizopo za mtu kuishi katika hifadhi ya Ngorongoro.

Kule hairuhusiwi kulima, hairuhusiwi kufanya biashara yoyote, kuendesha chombo cha moto wala kule hairuhusiwi kumiliki ardhi.

Je, watu wa aina hii wako huru kweli? Mimi nawafananisha na Wapalestina wanaoishi Ukanda wa Gaza ambao pia wako kwenye sheria kali huku wakiwa hawaruhusiwi kufanya mambo bila ruhusa ya Israel na hivyo eneo hilo kuitwa gereza la wazi (open prison).

Sehemu kama hiyo ambayo shughuli ya kiuchumi inayoruhusiwa ni ufugaji pekee, inaua vipaji na kunakuwa na mzunguko wa umaskini.

**WALIOHAMIA MSOMERA WANASEMAJE?**

Mzee Isaya Laltaika, baba mzazi wa Jaji wa mahakama kuu Dk. Eliamani Isaya Laltaika, ambaye ni pacha wa mhadhiri mwandamizi wa kitivo cha sheria, chuo kikuu cha Tumaini Makumira kilichopo Arusha anaeleza anavyofurahia maisha mapya ya yeye na familia yake baada ya kuhama kutoka Kijijini Nainokanoka Ngorongoro, kwenda Msomera.

Yeye, kama ilivyo kwa wenzake amepewa nyumba iliyopo katika eneo la ekari mbili na nusu na shamba kwa ajili ya kilimo na eneo la malisho.

"Faida niliyopata kuja Msomera. Kwanza ni ardhi, manake kule (Ngorongoro) tulikuwa hatumiliki ardhi, kwa hiyo sasa hivi nina ardhi ya kwangu mwenyewe ekari mbili na nusu na ekari nyingine tano ambazo naweza kulima," anasema Laltaika

Anaongeza: "Baada ya kuja hapa, tumepata miundombinu mingi tu ya huduma mbalimbali ikiwa tayari; maji, barabara, hospitali na umeme. Nashukuru kwamba kule (Ngorongoro), tulikuwa kifungo baridi, lakini sasa tumefunguliwa."

**WACHACHE**

Katika jamii yoyote, kuna watu wenye kasumba ya kuogopa mabadiliko hata yakiwa chanya namna gani.

Hawa ni watu wanaopenda kuishi kama walivyoishi mababu zao wakihofia kupambana na changamoto mpya.

Watu wa aina hii na mara nyingi wenye umri mkubwa, ndiyo wanaoendelea kuwa na hofu ya kuhama.

Lakini kupitia kwa wananchi hao katika moja ya vikao, walisema yapo mashirika na wanasiasa wachache, ambao kwa malengo yasiyofahamika au kwa kutafuta sifa, wamekuwa wakipitapita wakipotosha lengo la serikali la kuwahamisha wananchi hawa kwa hiari.

Kuna wanaodai serikali inawahamisha ili eti ilete mwekezaji.

Nina shaka watu hawa wachache, baadhi wakiwa wanasiasa, wanalenga kudanganya wananchi kwamba wao wanalinda haki zao hivyo wamekuwa wakipindisha ukweli katika kuwaeleza watu wa nje ikiwemo EU kuhusu zoezi zima ili kuipa serikali picha mbaya.

**NANI ASINGEFANYA KAMA SERIKALI?**

Ngorongoro ni hifadhi ambayo imekuwa moja ya vivutio vikubwa nchini, ikituingizia fedha nyingi kutokana na utalii.

Hata hivyo, ongezeko kubwa la watu na mifugo linatishia kupotea kabisa kwa mbuga hii ambayo mwaka 1979 iliwekwa katika orodha ya Urithi wa Dunia na Unesco, upande wa uhasilia.

Katika mazingira kama hayo, kunakuwa na machaguo mawili; kuiacha hii hifadhi ipotee au kuinusuru.

Namna nzuri ya kuinusuru, ni kuhamisha watu na mifugo yao kwenda sehemu nyingine kwa sababu maeneo yapo na haiwezekani kuhamisha wanyama na maliasili nyingine na bado ukabaki na hifadhi.

Lakini swali la kujiuliza ni hili. Katika mazingira ambayo Ngorongoro ilikuwa umefikia; idadi kubwa ya watu na mifugo kwenye hifadhi, kama hifadhi hii ingekuwa katika moja ya nchi zinazounda EU wasingechukua hatua kama inavyochukua serikali yetu?

Wakati serikali yetu inajipanga kujenga Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere katika lililokuwa pori la akiba la Selous, hawa wadau wetu wa maendeleo (nchi za EU) walipingapinga wakidai litaharibu mazingira na uasili wa pori hilo.

Kama ndivyo, mantiki inaonesha walipaswa kuungana na serikali kwa hili inalolifanya katika kuokoa Ngorongoro.

**NINGEKUWA NA MAMLAKA**

Kama ningekuwa mimi (mwandishi wa makala haya) ndiyo mwenye mamlaka, kuhamisha watu katika hifadhi ya Ngorongoro na kubakiza wasiozidi milioni 20 huku kila wanapoongezeka baada ya miaka fulani nawahamisha waliozidi ingekuwa ni lazima, siyo hiari!

Labda suala lingekuwa ni utaratibu gani ungetumika kuwahamisha na wachache kubaki. Je, ni kwa kupiga kura, kuangalia umri au kile ambacho wananchi wangeamua.

Au ningewahamisha wote kwa sababu maeneo ya kwenda yapo na kuruhusu wanaotaka kurudi kwa hiari wafanye hivyo na idadi sahihi ikishafika, basi.

Sababu za kufanya hivyo ni nyingi, moja ni kwamba serikali inapoona eneo linafaa kwa uwekezaji au matumizi fulani na manufaa yake kwa nchi ni makubwa, pamoja na kuheshimu haki za kimataifa za watu kuishi katika maeneo yao ya asili, imekuwa ni kawaida kuwahamisha wananchi na kuwalipa fidia. Serikali zote duniani zinafanya hivyo.

Kwa mfano, wakati wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam, hapakuwa na hiari ya kuhama!

Swali, kuna mji au eneo hapa nchini ambalo watu hawajahamishwa kwa ajili ya kupisha shughuli fulani ya maendeleo kama upanuzi wa barabara au uwekezaji mwingine?

Pale Geita, nakumbuka, mahali uliko leo mgodi wa dhahabu wa Geita Gold Mine Limited (GGML), kulikuwa na Kijiji cha Mtakuja, lakini kwa ajili ya kupisha uwekezaji mkubwa ambao unazalisha ajira nyingi na mapato kwa serikali wananchi walihamishwa na kama kawaida wahafidhina walipingapinga.

Waliohamishwa kutoka Mtakuja, mbali na kulipwa fidia ya nyumba na mashamba yao, hawakujengewa nyumba wala kingine chochote, lakini leo wapo wengi wanaofaidi matunda ya uwekezaji huo mkubwa moja kwa moja au kupitia huduma za kiserikali.

Katika eneo ambalo, zaidi ya kuchunga ng'ombe watu huwaruhusiwi kulima, kumiliki ardhi, kufanya biashara wala vijana kuendesha bodaboda ni sahihi kweli kuendelea kuwaacha katika hali hiyo ya umasikini badala ya kuwapeleka kwenye maeneo yenye fursa nyingi za kimaendeleo? Mimi naona si sahihi na ndiyo maana ningekuwa na mamlaka ningewahamisha bila hiari na kuna siku wangenishukuru!

**KUPONGEZWA**

Kwa kile kinachofanywa na serikali kwa kuwahamisha kwa hiari 'kama wafalme' kulinganisha na wenzao ambao walishahamishwa na serikali katika maeneo mbalimbali, mimi naona, walipaswa kuipongeza serikali badala kuinyooshea kidole.

Ingawa zipo serikali za kibabe Afrika, za viongozi wasio na huruma, madikteta, wasiojali haki za bindamu na ambao hawajali wananchi wao kuteseka, lakini Serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kwa kuazima maneno ya Mwalimu Nyerere alipomzungumzia Rais Ali Hassan Mwinyi, huwezi siku moja ukawa umekaa mbele ya Rais Samia kisha ukasema: "Sasa niko mbele ya Rais mbabe, asiye na huruma, dikteta na mvunja haki za bindamu." Huwezi.

Ukisema hayo, haki-ya-Mungu utakuwa unamwonea.

Siasa



# Amani yetu inawakera mahasidi, tusiichezee

**Na Hamid Yassin**

MIAKA kadhaa huko nyuma mikusanyiko ya kidini ndiyo ilikuwa inatishia amani na utulivu wa nchi yetu. Lakini sasa wameibuka wanasiasa pasua kichwa wanaotaka kuturudisha kule kule.

Hivi karibuni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya kufungua tawi jipya la chama hicho pale Tabata Kisiwani Makaburi kata ya Mabibo ambako kwenye hotuba yake alitoa kauli zenye viashiria vyote vya uchochezi.

Katika shughuli ile ambayo pia ilihudhuriwa na wanachama wa Chadema kutoka majimbo ya Ubungo na Segerea, Lissu aliwaambia wenzake kwamba eti sasa nchi inakwenda mahali pagumu na kuwataka wajiandae kwa lolote litalotokea!

"Tusikubali kuchekewa na kukenuliwa meno, mjiandae kwa mapambano ya mbele, narudia ni kugumu, alihutubia Lissu huku wafuasi wa chama hicho wakimjibu kwamba wamemwelewa."

Wenye akili zetu tunaelewa Lissu anamaanisha nini kutoa kauli hizo katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa hapo mwakani na ule Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025!

Anataka kuanza kujenga dhana kwamba chaguzi hizo hazitakuwa huru na haki hivyo wajiandae kufanya vurugu!

Kumbuka hii ni mara ya pili katika kipindi kifupi Lissu anazua tafrani baada ya kufanya hivyo kule Arusha na Manyara na kisha kudhibitiwa na vyombo vya dola asieneze uchochezi wake kwa kabila la Wamasai wa kule Ngorongoro dhidi ya Serikali yao tukufu iliyo chini ya Mama msikivu, Dk. Samia Suluhu Hassan

Wakati Lissu anafanya hivyo hapa Dar, kule Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kaskazini na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Godbless Lema hivi karibuni alikuwa anazunguka mitaani na kujitwisha majukumu ya kusikiliza na kutatua kile alichoita kero na unyanyasaji wanaofanyiwa wananchi na serikali yao!

Zipo klipu za video zinamwonesha Lema akizunguka mitaani na kundi kubwa la watoto na akina mama kisha anaingia kwenye baadhi ya nyumba za wakazi hao wa Nkasi ambao wanalia huku wamejifunika gubigubi wasionekane sura zao.

Kilichonishangaza akina mama wale waliokuwa wakilia na kuficha sura zao walikuwa hawasemi hayo masahibu yaliyowafika zaidi ya kulia huku kada mmoja mwanamke wa Chadema akiongea mambo yasiyoeleweka vizuri kwa niaba yao!

Hivi kweli viongozi wote wa Wilaya ya Nkasi na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wao wameshindwa kutatua matatizo yaliyowakumba akina mama wale kama kweli yapo mpaka wamkabidhi jukumu hilo Lema?

Lema huyu ambaye yeye mwenyewe anashindwa kukabili matatizo yanayomkumba hadi wakati mwingine kukimbia nchi eti kwa usalama wake!

Huu ndiyo uhuru waliokuwa wanalilia wapinzani? Yaani chama kinajengwa kwa kugombanisha wananchi na serikali yao!

Wapinzani wapo tayari yao yatimie hata kama itagharimu kupoteza amani na utulivu wetu tulioujenga na kuulinda kwa miaka mingi sasa!

Tanzania neno amani linaeleweka na kada zote. Kwa Watanzania halihitaji elimu kwani wanalielewa kwa mapana yake.

Jambo la amani halihitaji tafsiri bali kila mtu anaihitaji amani; kila kitu kitafanyika chini ya amani kubwa katika maisha ya mwanadamu ni maendeleo na kumcha Mungu.

Kitu cha ajabu ni kwamba, amani yetu tumeanza kuichezea na wala hatuna shaka ya kutaka kuweka maisha yetu hatarini. Tunataka kufikishana mahali ambapo tusiwe na uhakika na leo yetu kwa kuhofia ni tukio gani litatokea baada ya muda mfupi ujao!

Na wala hatujali kuwa kama leo yetu haipo salama hata kesho yetu imepungukiwa. Haya yote yanafanyika kwa sababu ya wanadamu ambao kwa utaifa wetu baadhi yetu wameamua kufuta historia na uhalisia tulioachiwa au kukulia na kulelewa kwayo.

Amani ni mtaji unaotafutwa na nchi nyingi duniani lakini kwa bahati nzuri, amani ipo katika nchi ambazo zimetambua mapema na kulea watu wake katika misingi hiyo ya utulivu na amani.

Katika kipindi chake hiki kifupi madarakani, Rais Dk. Samia, ameonya na anaendelea kukemea mara zote wale wanaotaka kuichezea amani, usalama na utulivu uliopo nchini kwetu.

Rais ananasihi mara kwa mara; "Amani yetu ndiyo karaha kwa watu wengine, nawaomba sana Watanzania tusiichezee amani yetu ikipotea tutajuta".

Rais Dk. Samia anatambua amani hupandwa na kuchipuka katika jamii yeyote ambayo imetambua thamani yake, hivyo amani ipo ndani ya uhalisia wa watu. Hata hivyo, kuna baadhi ya watu ambao ni tofauti na makuzi ya amani kutokana na sababu zao binafsi ikiwa ni pamoja na umimi, asili ya jamii husika, mila na desturi na utashi wa mtu mwenyewe.

Usemi wa Rais unaakisi hali halisi ya watu wachache waliopo ulimwenguni ambao hawapendi nchi yetu iwe na amani, kwao jambo lolote baya linalojitokeza hulifanya mtaji ili kupenyeza yale waliyokusudia. Lakini unapolitambua hili kama nchi haisumbui, tatizo ni kwa wale wasiochambua na kuelewa mambo, wao hulichukua kama lilivyo na kuliamini.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alisema; "Serikali ya Tanzania haina dini, ila watu wake wana dini. Kila mtu ana haki ya kuabudu na kufuata dini anayoitaka ili mradi havunji sheria".

Dini zetu kubwa hapa Tanzania zinahimiza kuilinda na kuienzi amani yetu, ili tupate nafasi ya kumcha Mungu, kupendana kushirikiana kuwa na umoja, masikilizano, na ushirikiano.

Hata hivyo, wapo baadhi ya wachache katika jamii zetu kwao kukosekana kwa amani ni mtaji wa kufanikisha mambo yao.

Kutapokuwa hakuna amani kila mmoja atatetea nafsi yake, uhai wake, uwepo wake, maslahi yake, matarajio yake sambamba na nafasi yake katika jamii.

Pasipo na amani mtu hana nafasi ya kukumbuka familia yake ingawa wakina mama mara zote huwajibika kutetea maisha yao na watoto wao.

Watanzania tusichezee amani tuliyonayo, mauaji ya kimbari nchini Rwanda, yalichochewa na baadhi ya vyombo vya habari, ambavyo vilidhani vinatimiza wajibu wake wa kutoa habari kumbe ikawa ndio sehemu ya kuwasha moto wa mauaji".

Kukosekana kwa amani sio wimbo au pambio ambalo huvutia kusikiliza katika masikio, ni vigumu sana kwa baadhi ya watu kugundua alilolitenda au kusema ndio mwanzo wa kupotea kwa amani.

Amani ndio chanzo cha tafsiri pana inayobeba maisha ya wanadamu na mustakabali wa kutumia kila kitu kilichopo duniani kwa ustawi na kujiletea maendeleo.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere pia aliwahi kusema kwamba, viashiria vya uvunjifu wa amani ni pamoja na ukabila, udini, ubaguzi wa aina yoyote, dharau, kumiliki rasilmali za taifa peke yako ambao ni aina ya upungufu wa fikra.

Mara nyingi Mwalimu Nyerere hakuchelea kutambua viashiria vya kuvunja amani vya aina mbalimbali na kuvifanyia kazi mara moja kabla madhara hayajawa makubwa kwa mtu mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mfano mwaka 1967 alipowahutubia wazee na wananchi wa Dar es Salaam akifafanua kwa nini aliwafukuza wanafunzi 393, walioandamana wakipinga Mpango wa Jeshi la Kujenga Taifa, alinena kwamba ilikuwa nia njema ya kuandaa Taifa linalojitambua lenye uzalendo, ambalo vijana wako tayari kulinda usalama wa nchi, masilahi yake na rasilimali zilizopo kwa manufaa ya Watanzania ili kuleta maendeleo na kujenga Taifa imara na madhubuti.

Tafsiri hiyohiyo ya Baba wa Taifa ndiyo anayoitumia Rais Dk. Samia ya kukemea na kuwasihi Watanzania kuitunza amani yetu kama mboni ya jicho. Maana ikitoweka haitawezekana kuirejesha, kwani wapo watakaojitolea kwa hali na mali ili isirejee kwa kuwa wanajua amani inapokosekana watapata wanachokusudia.

Watanzania ni vyema tuchukue tahadhari na kumtanguliza Mwenyezi Mungu mbele katika kuilea amani yetu, ambalo ndio hitaji kubwa kwa Watanzania wa vizazi vya sasa na vijavyo.

Tanzania pia inatamani kuwa Taifa kubwa miaka dahari ijayo lenye historia itakayoipendeza dunia na kuwa mfano wa kuigwa.

Tukumbuke amani yetu ni mtaji, wengi wanaitafuta kwa udi na uvumba, lakini haikamatiki, hata kama Taifa lako lina fedha nyingi za kupindukia huwezi kuinunua amani. Hata kama Taifa lako lina wanasiasa wazuri kiasi gani huwezi kuirudisha amani iliyotoweka.

Amani ni mtaji unaowaleta wawekezaji wa aina mbalimbali hapa Tanzania sio kwa sababu Tanzania ina rangi nzuri kuliko nchi nyingine la hasha, ila ni kwa sababu ya mtaji muhimu na mkubwa kuliko yote na wa kipekee tuliojaliwa na Mwenyezi Mungu wa amani.

Ni muhimu kujiuliza nini cha kufanya ili kuweza kuikumbatia amani yetu na kuendelea kuilea miaka na miaka. Majibu ni rahisi kwa kuwa misingi imara na miongozo tulishawekewa na Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na viashiria tunavijua, tuhakikishe tunapiga vita kwa nguvu zote ili kuilinda na kuenzi amani yetu ambayo ni hitaji letu namba moja.

*Mawasiliano ya Mwandishi wa makala haya ni 0768 888 787*

# Tatizo la kutokwa jasho jingi na namna ya kulidhibiti

**Na Godfrey Sanga**

UMEWAHI kukutana na mtu na kusalimiana naye kwa kupeana mikono na ukahisi majimaji mkononi baada ya salamu? Je, ulijiuliza maji hayo yametoka wapi?

Ukweli ni kwamba hayo si maji bali ni jasho linalotoka katika viganja vya mikono ya mtu huyo uliyesalimiana nae. Hii kitabibu hujulikana kama palmoplantar hyperhidrosis. Ni hitilafu katika mwili inayosababisha mtu kutokwa na jasho kupita kiasi viganjani.

Siyo viganja pekee, wapo wenye tatizo la kutoka jasho jingi katika maeneo ya kwapani na katika nyayo za miguu. Hii hujulikana kitabibu kama axillary hyperhidrosis

Mbali na hao, wapo wengine ambao wenyewe wana hitilafu hii ya kutokwa jasho kupita kiasi, hasa maeneo ya usoni, katika kiwiliwili, maeno ya tumboni, mgongoni na kifuani.

Kutokwa jasho kupita kiasi mwilini ni dosari ya kawaida na si tishio la kiafya au linalohatarisha maisha ya mtu lakini ni jambo linaloweza kumnyima mtu furaha.

Kwa kawaida jasho la mwili huwa ni mchanganyiko wa majimaji, chumvichumvi za mwilini, kemikali za amonia na urea ambayo ni mabaki baada ya protini kuvunjwavunjwa mwilini.

Mara nyingine utokaji huu wa jasho unaweza kumnyima mtu uhuru wa kujumuika katika mambo ya kijamii ikiwamo kujichanganya na wana jamii wenzake, kufanya biashara hata kutafuta elimu.

Tatizo hili linaweza kuonekana kwa vijana ambao wako katika umri wa balehe na wengi wanapata tatizo la kutokwa na jasho kupita kiasi maeneo ya makwapani.

Hii inaweza kuwasababishia matatizo ya kijamii na kisaikolojia, kwani wenzao wanaweza kuwatenga na kuwanyanyapaa na kuwafanya kujichukia, kuchukia mazingira na hali hiyo kwa jumla na hata wengine kukacha masomo.

Dosari hii ya utokaji wa jasho kupita kiasi inaweza kuwashtua wanajamii wakidhani mwathirika ana tatizo kubwa la kiafya, bila kujua kuwa tatizo hili linawapata watu lakini wakiwa wako imara kiafya pia.

Wazazi nao wanaweza kuona hali hii kwa watoto wao wadogo si ya kawaida na hasa katika majira kama ya kipindi hiki cha joto katika maeneo kama ya Pwani ambapo fukuto ni kubwa na utokaji wa jasho huongezeka maradufu.

Wapo wengine hudhani labda mtoto kapata homa kali na hivyo huwakimbiza katika maeneo ya huduma za afya.

Chanzo cha mtu kutokwa na jasho la mwili kupita kiasi kinaweza kuwa ni mfumo wa fahamu, shughuli za ndani ya mwili na magonjwa yanayojitokeza mwilini kiujumla ikiwamo malaria na shinikizo la damu.

Pia, yapo mambo yanayoweza kuchochea utokaji jasho kupita kiasi kama vile mtu kuwa katika mazingira ya joto kali na mabadiliko ya kihisia ikiwamo kukasirika, kupata taarifa za kushtua, hofu na wasiwasi lakini hata matumizi ya badhi ya dawa na vyakula.

Chini ya ngozi ya mwanadamu zipo tezi za jasho za aina tatu. Tezi hizo hupata taarifa kutoka kwenye ubongo na mishipa midogo ya fahamu iliyopo chini ya ngozi na kuchochea hali ya kuruhusu jasho kutoka.

Vilevile homoni za mwili wakati wa shinikizo au mabadiliko ya hisia nazo huzipa ishara tezi hizo kutoa jasho.

Katika ubongo kipo kituo kinachohusika na kudhibiti joto la mwili, eneo hili lina mawasiliano na tezi hizi pale joto linapokuwa kali ambalo huamrishwa na ubongo kutoa jasho ili kupooza mwili.

Katika mwili wa mwanadamu kuna karibu tezi za jasho milioni nne huku kati ya hizi milioni tatu ni za aina ya acrine gland ambazo ndizo zinahusika katika kudhibiti joto kali la mwili. Zina kazi ya kutoa majimaji yasiyo na harufu ambayo husaidia mwili kuweza kupooza joto la ndani kwa njia ya mvuke wa joto hivyo kupooza joto la mwili.

Kwa kawaida jasho huwa halina harufu isipokuwa bakteria wa kwenye ngozi au kwenye nguo ndio wanaweza kushambulia jasho na kusababisha litoe harufu.

Na kwa kawaida, tezi za jasho zilizopo viganjani na nyayoni huchochewa kutoa jasho pale kunapokuwa na mabadiliko ya hisia za mwili. Ndio maana wenye tatizo la kutokwa jasho jingi viganjani na nyayoni hujikuta wakiwa na hofu.

Kwa upande wa wale wanaotokwa jasho zaidi maeneo ya kwapani, tezi za jasho zilizopo kwapani huchochewa zaidi na mabadiliko ya joto la mwilini ambalo hudhibitiwa zaidi na ubongo. Halikadhalika, mabadiliko ya hisia huchochea jasho kutoka kwa wingi kwapani.

Mara nyingine tatizo hili kwa kiasi kikubwa huwa si la mara kwa mara na linaweza kutibiwa kama litaonekana kero kwa mtu japo mhusika anaweza kupata ushauri hasa katika kuboresha usafi wa mwili ili kuepukana na harufu mbaya baada ya bakteria kushambilia jasho.

Hata hivyo, kabla tatizo halijatibiwa ni lazima wataalamu wa afya walitathimini kubaini chanzo kinachochea tatizo hilo. Watatazama eneo la mwilini lenye tatizo hili na pia kupima ukubwa wa tatizo.

Lakini kwa nchi zilizopiga hatua kimaendeleo watu wenye tatizo hilo hupewa matibabu ya vyakula au virutubisho vyenye viambata asilia ambavyo vina uwezo wa kupunguza jasho kutoka.

Zipo dawa zijulikanazo kama Anticholigenic ambazo mwathirika hupewa. Hizi zinafanya kazi ya kuingilia mfumo wa fahamu katika kutotitirisha kemikali zinazosaidia taarifa kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Ipo dawa nyingine ijulikanayo kama Botox iliyothibitishwa na taasisi ya dawa na chakula ya nchini Marekani ambayo pia hutumika kwa ajili ya kupambana na tatizo la kutokwa na jasho kupita kiasi katika maeneo ya kwapani.

Upasuaji pia unaweza kufanyika kwa kuiziba mishipa ya fahamu inayopeleka taarifa katika eneo la ngozi lenye tezi zinazotoa jasho. Vilevile kinaweza kufanyika upandikizaji wa ngozi katika eneo lenye tezi za jasho zinazotoa jasho kupita kiasi.

Jambo la msingi kwa mtu mwenye tatizo hili ni kuhakikisha anakuwa msafi wa mwili. Ni vyema awe akivaa nguo zenye malighafi za pamba kwani ni rahisi kunyonya jasho mbali na kupunguza kuchochea jasho.

Inashauriwa pia kuvaa nguo zenye rangi ambazo hazisharabu mwanga wa jua ili kuepukana na uhifadhi wa joto. Nguo nyeusi na bluu, kwa mfano ndizo zinazohifadhi joto na kuchochea jasho kutoka kwa wingi kutokana na kusharabu mwanga.

Lakini kwa wale wanaonuka kikwapa (bromhidrosis), mbali na kushauriwa kufanya usafi mara kwa mara na kusafisha kwapa na kujitia uturi, zipo njia za kiasili ambazo husaidia kudhibiti harufu.

Baadhi ya vitu asilia anavyoweza mtu kutumia ili kuondoa harufu hiyo mbaya ni limau au siki ya tunda la tufaha.

Mtumiaji anatakiwa kwanza kunyoa makwapa kisha kuoga kwa maji safi.

Kisha akachukua kipande kimoja cha limao na kusugua kwapani na cha pili kwapa la pili.

Atafanya hivyo kila siku hadi pale atakapoona shida ya kunuka imeisha.

Hata hivyo mtu mwenye ngozi iliyo na matatizo hashauriwi kutumia limau kutokana na kemikali iliyo katika tunda hilo.

Huyu anaweza kutumia siki ya tufaa. Huyu baada ya kuoga atachukua kipande cha pamba na kukichovya katika siki kabla ya kusugua kwapani akitumia pamba hiyo.

Anayetumia atafanya hivyo mara mbili kwa siku hadi pale atakapoona mabadiliko.

Zipo taarifa pia za watu kutumia ukoko wa ugali na maji ya mchele kutibu tatizo la kikwapa. Jaribu itakayokusaidia.

*Makala hii imeandikwa na Godfrey Sanga kutokana na vyanzo mbalimbali.*



Siasa



# Samia anavyotoa majibu sahihi kwa wahafidhina -2

**WIKI iliyopita katika makala hii tuliangalia baadhi ya kazi ambazo zimekuwa zikifanywa na Rais Dk Samia Suluhu Hassan na kutoa majibu sahihi kwa wahafidhina kwamba chini iko katika mikono salama na 'kazi inaendelea' katika kiwango cha juu.**

Baadhi ya kazi hizo za Dk. Samia zinazoongea ambazo tuliziangalia ni pamoja na kufanya maridhiano katika nyanja ya siasa ambapo kwa nyakati tofauti amekutana na viongozi wa vyama vya siasa.

Pia tukaona namna anavyoendeleza au kuanzisha miradi mipya ya kimkakati. Miradi hiyo ni kama ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Nyerere (JNHPP), reli ya kisasa (SGR), Daraja la Magufuli, bandari ya Uvuvi Kilwa, uboreshaji wa shirika la ndege (ATCL) na kadhalika na kadhalika.

Kazi nyingine zilizofanywa na kuwanyamazisha wahafidhina ni uboreshaji wa sekta ya madini, kupaisha sekta ya utalii kupitia filamu ya The Royal Tour, uboreshaji wa diplomasia ya uchumi na kadhalika.

## UHURU WA VYOMBO VYA HABARI

Mbali ya maendeleo makubwa yaliyopatikana ndani ya muda huu mfupi wa takribani miaka miwili na nusu, kumekuwa na uhuru mkubwa wa habari kwenye Serikali ya Awamu ya Sita tofauti na ilivyokuwa wakati wa Awamu ya Tano.

Ujenzi wa Tanzania ya Kidijiti umeendelea kuboreshwa, hatua ambayo pia inanyanyua kwa haraka maisha ya Watanzania sambamba na kutoa fursa mbalimbali.

Tumeshuhudia uhuru maridhawa wa vyombo vya habari ambapo kupitia tamko alilolitoa Rais Samia Aprili 6, 2021 la kuiagiza iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuvifungulia vyombo kadhaa vya habari na kuwataka watendaji waepuke kuvishughulikia kwa namna ambayo inaweza kusababisha serikali kulaumiwa kwa kuminya uhuru wa habari.

Rais Samia alisema, "Wizara ya Habari, mnapaswa kusimamia vyombo vya habari, nasikia kuna vyombo vya habari huko mmevifungia, vifungulieni lakini vifuate sheria na kanuni."

Agizo lile la Rais Samia linadhihirisha namna ambavyo serikali yake ilivyodhamiria kujenga Tanzania ya uhuru wa kuzungumza na Tanzania ya Kidijiti

Katika hotuba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa 2022/23 alisema

utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo kutaiwezesha Tanzania kuimarika kushiriki uchumi wa kidijiti katika kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4th Industrial Revolution) .

Wizara hiyo mbali na jukumu la kutunga na kusimamia sera zinazohusiana na masuala ya habari, mawasiliano, na teknolojia ya habari, ina dhima pia ya kuratibu na kusimamia vyombo vya habari, na mawasiliano ya posta na simu.

Vilevile, inaendeleza wataalamu, tafiti na ubunifu kwenye masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kuendeleza na kusimamia miundombinu ya mawasiliano nchini.

Hata katika hotuba yake, Nape alisema serikali imeendelea kuweka miundombinu yenye kuruhusu ukuaji wa uhuru wa habari katika ujenzi wa Tanzania ya kidijiti.

Agosti 19, 2021, wizara hiyo ilifanikisha kusainiwa kwa mkataba kati ya Serikali na Benki ya Dunia wenye thamani ya dola za Marekani milioni 150 ambapo mradi ulianza kutekelezwa Novemba, 2021 ukilenga kuboresha na kukuza maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kuweza kufikisha huduma za Watanzania kuwa na wigo mpana wa kutoa mawazo yao juu ya masuala mbalimbali.

Na mara kadhaa Rais Samia amekuwa akikumbusha; "Tukosoeni kwa staha na mie nashauri ni vyema tukaishi katika nyakati za utu na ustaarabu".

## DK. SAMIA NI NANI?

Samia Suluhu Hassan alizaliwa Januari 27 mwaka 1960. Ni Rais wa sita wa Tanzania.

Kabla ya kuwa rais kutokana na kifo cha Rais wa Tano, John Magufuli, kilichotokea tarehe 17 Machi 2021, Suluhu alikuwa Makamu wa Rais kwa sababu ya kuwa mgombea mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa 2015.

Ni rais wa kwanza mwanamke na rais wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar, wa kwanza alikuwa ni Ally Hassan Mwinyi, Rais wa awamu ya Pili.

Aprili 30 mwaka 2021 alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa chama tawala (CCM) huku akiwa mwenyekiti wa kwanza mwanamke.

Alisoma shule za msingi za Chwaka hapo Unguja, Ziwani kule Pemba na Mahonda (Unguja) katika miaka ya 1966 hadi 1972. Aliendelea na masomo ya sekondari shule za Ng'ambo, Unguja (1973-1975) na Lumumba, Unguja (1976).

Baada ya kumaliza masomo yake ya sekondari mnamo 1977, aliajiriwa na Wizara ya Mipango na Maendeleo kama karani. Alisoma kozi fupi kadhaa. Mnamo 1986, alihitimu diploma ya juu katika utawala wa umma kutoka Taasisi ya Usimamizi wa Maendeleo (sasa Chuo Kikuu cha Mzumbe ).

Baada ya kuhitimu, aliajiriwa kwenye mradi uliofadhiliwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (World Food Programme). Kati ya mwaka 1992 na 1994, alisoma kwenye Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza na kuhitimu stashahada ya uzamili katika uchumi.

Mwaka 2000 aliamua kujiunga na siasa. Aliteuliwa na CCM kama mbunge wa viti maalumu katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar akateuliwa na rais Amani Karume kuwa Waziri wa Utalii na Bishara. Alichaguliwa tena mnamo 2005 kwenye viti maalumu na aliteuliwa tena kama Waziri katika Wizara ya Kazi, Jinsia na Watoto.

Mwaka 2010 aligombea kwenye uchaguzi wa Bunge la Kitaifa, akisimama katika jimbo la Makunduchi na kushinda kwa zaidi ya asilimia 80. Rais Jakaya Kikwete alimteua kuwa Waziri wa Nchi anayeshughulikia Mambo ya Muungano.

Mwaka 2014 alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba lililokuwa na jukumu la kuandaa katiba mpya ya nchi.

Mnamo mwaka 2015, alipata shahada yake ya pili (MSc) katika Maendeleo ya Uchumi wa Jamii kupitia mpango wa pamoja kati ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Kusini mwa New Hampshire.

*Kwa maoni; 0768 888 787*




Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Anza hata kabla hujawa tayari



UTAPATA nguvu kubwa ya akili baada ya kuanza.

Moja kati ya vitu ambavyo vimekuwa vinawakwamisha wengi wasiingie kwenye biashara au kutekeleza malengo yao mbalimbali, ni kutokuwa tayari. Unawezakuta mtu analo wazo na hajafikia ukamilifu wa asilimia mia kutosha kuanza. Inawezekana hajapata kila anachohitaji ili kuanza, n.k.

Sasa kwa kuwa anakuwa hajawa tayari, anaona ni sahihi kwake kuendelea kusubiri na anaendelea kujifariji kuwa ni sahihi kwake kutokuanza jambo kwa sababu bado hajapata kila ambacho anataka kuwa nacho ili aanze.

Kwa kawaida hilo linaweza kuonekana sawa, lakini kwa upande wa mafanikio siyo sawa. Hakuna wakati ambao utakuwa tayari kwa kila kitu ndiyo uanze. Kila wakati kuna kitu utakuwa unakosa au kuna kitu kitakuwa hakijakamilika. Njia pekee ya kuanza biashara au kutekeleza mipango yako ya kufanikiwa, ni kutokusubiri kuwa tayari kwa kila kitu, unatakiwa kuanza.

Kwenye maisha, tatizo huwa si kupata mawazo, mipango au malengo.

Haya yanapatikana kwenye utulivu na ubunifu ambavyo hufanywa na uwezo wetu wa kupanga mambo. Tatizo kubwa ni kuhamisha mpango toka kichwani, kuja kwenye karatasi (Project write up) na kuufanya uwe halisi.

Mara nyingi hii inatokea kwa mtu mmoja au taasisi kuwa na mipango mizuri lakini kushindwa kuitekeleza, Lakini sababu zipo nyingi zinazofanya mipango ya mtu au taasisi isifanikiwe. Tutapitia sababu kadhaa hapa zinazofanya mipango kushindikana kutekelezeka.

Sababu ya kwanza ni matokeo ya kitabia au utamaduni: Kuna watu wameshajenga utamaduni au tabia ambazo zinawazuia kufikia malengo kwa kutekeleza mipango. Tabia hizi ni kama ugumu wa kukubaliana na mabadiliko (culture of resistance to change), kukosa imani na mchakato, nk. Unaweza kujiona kila siku unapanga na hutekelezi na ukawa hujui kwa nini unabakia hapohapo siku zote.

Inawezekana ndani yako unapanga mambo lakini hata wewe hujabalisha mtazamo wako uliojengewa na utamaduni au tabia zako. Maana yake mpango wako unakinzana na mtazamo wako bila wewe kujua. Au unapanga kitu kwa akili lakini ndani ya mtazamo wako mwenyewe huamini kama unaweza kuwa vile ulivyopanga.

Waafrika wengi tunakwama hapo. Tunaweza kupanga kwa kuona mafanikio mahali bila kujua kwamba ili kufika pale kunahitaji mabadiliko ya kifikra kwanza ambayo yataambatana na mabadiliko ya kuondoa utamaduni wa awali kichwani.

Sababu nyingine ni kutoshughulika kuondoa vikwazo: - Wakati wa kuanza utekelezaji, watu au mashirika hukutana na changamoto au vikwazo kadhaa maalum. Kutambua na kushughulikia changamoto hizi ni muhimu ili kutekeleza mkakati/mawazo kwa ufanisi. Tatizo kubwa ni kutokuwa na uwezo au nguvu ya kutatua changamoto hizo. Mfano mtu anawezajiona kanakwamba kuna vitu havijakamilika, sasa anachagua kuamua kusubiri kila kitu kikamilike ndipo aanze utekelezaji.

Waliofanikiwa wote hawakusubiri mambo yakamilike, waliamua kuanzia pale walipo kisha wanakamilika hatua kwa hatua.

Sababu nyingine ni kutokuwa na maono na lengo wazi (Vision and Mission): - Kuanzisha jambo hakuhitaji tu wazo, bali kunahitaji maono na dhamira ya dhati na ya wazi. Maono na dhamira ni hatua ya kwanza kuelekea utekelezaji mafanikio wa mkakati. Taarifa ya maono inaelezea matamanio ya mtu au shirika na kile unachotaka kufikia kwa muda mrefu.

Kwa upande mwingine, taarifa ya lengo inafafanua kusudi la mtu na jinsi anavyopanga kufikia maono yake. Sasa watu wengi haya mambo hata hawayajui na hata hawajui kama yana umuhimu kiasi gani na ndiyo maana hata hawahangaiki kutafuta washauri (Consultants) kwa ajili ya maisha yao wenyewe. Hii ni dalili ya wazi kwamba wanaona kama vile maisha yao yapo sawa na hakuna madhara. Tabia hii inatufanya kuendelea kuishi chini ya kiwango siku zote.

Wework Consult - Your Partner in Growth.



Na Hamisi Kibari

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 12

**Chris anampiga mkewe akimtetea hawara yake hadi anapoteza fahamu. Baadaye analazimika kumpeleka hospitali akiwa hajitambui. Anawadanganya ndugu wa mkewe kwamba mwanamke huyo ametoweka. Daktari anamjulisha kwamba mkewe amefariki dunia, kisha anampa njia itakayosaidia asishitakiwe kwa mauaji. Chris anakubali njia hiyo lakini gharama za kuficha kifo hicho ni kubwa. Chris anayewahadaa ndugu za mkewe kwamba yuko katika harakati za kumtafuta, hatokei katika kikao muhimu cha kujulishana mahala alikofikia katika kumtafuta. Wakati ndugu wa mkewe sasa wakiwa kiguu na njia polisi, Chris anatafuta nyumba ya kupanga. Imekuwaje? Fuatana na mtunzi katika kisa hiki.**

"Kuna wapangaji watatu tu. Wawili wamepanga mabanda ya nyuma na mmoja ndo anaishi ndani (kwenye nyumba kubwa)," akajibu baba huyo mwenye nyumba, mfupi na mwenye upara.

"Ee...sasa tunaweza kukaa wapi ili tuandikiane mka..."

"Samahani kidogo, naomba tuongee faragha kwanza kabla hamjafikia kuweka mikataba," Joyce alimkatisha.

Joyce alimvuta Chris, wakasogea pembeni. Akaongea naye kwa sauti ya chini: "Hii nyumba gani? Mimi siwezi kuishi humu. Nyumba ina wapangaji kibao. Maana yake ni kwamba hivyo vyumba vingine viwili navyo vinasubiri wapngaji. Wapangaji wakipatikana itakuwa vurugu mechi humu ndani nguo kuchanika. Halafu nyumba yenyewe ya kizamani sana. Angalia rangi ilivyo, hata akipaka rangi mpya nyumba haiwezi kupendeza. Tutaishije humu?"

"Lakini mimi naona hii nyumba si mbaya sana na bei yake ni nzuri," alijibu Chris.

"Aku babu, hapa utaishi mwenyewe. Nyumba gani hii?" Akasema tena Joyce akibetua midomo yake iliyokuwa umepakwa rangi nyekundu iliyokolea mithili ya damu.

"Sikiliza mpenzi, sasa tutafanyaje wakati kesho kutwa inabidi tuondoke pale nyumbani. Yule daktari ambaye ni kama ametudhulumu nyumba anataka kuikarabati haraka. Tunafanyaje?"

"Tutatafuta nyumba nyingine ya maana. Wakati tukitafuta nyumba tutakuwa tunaishi hoteli," alijibu Joyce.

"Mbona tulikubaliana tufanye mkakati wa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima? Unadhani kuishi hoteli tutaongeza matumizi ama tutapunguza ili hizi fedha tulizobaki nazo zikamilishe malengo yetu?"

"Ndani ya wiki moja tutakuwa tumepata nyumba nzuri maeneo mengine... Hata mimi mwenyewe nitatafuta."

"Sasa huyu bwana wa nyumba tutamwambiaje?"

> **Hii nyumba gani? Mimi siwezi kuishi humu. Nyumba ina wapangaji kibao. Maana yake ni kwamba hivyo vyumba vingine viwili navyo vinasubiri wapngaji. Wapangaji wakipatikana itakuwa vurugu mechi humu ndani nguo kuchanika. Halafu nyumba yenyewe ya kizamani sana. Angalia rangi ilivyo, hata akipaka rangi mpya nyumba haiwezi kupendeza. Tutaishije humu?**

"Tutamwambiaje! Kwani lazima tupange kwenye hii nyumba. Tumwambie tunaenda zetu kwanza labda tutarudi baadaye tukiona inafaa kufanya hivyo... Au tumwambie tu derect kwamba hatujaipenda nyumba."

Chris aliafikiana na Joyce kuachana na hiyo nyumba ili watafute nyingine. Akamfuata mwenye nyumba aliyekuwa akiwasubiri wakati wanavutana pembeni. Akamweleza mbele ya dalali kwamba nyumba wameiona, si mbaya, lakini wameona wakashauriane kwanza kabla ya kuingia mkataba endapo wataona inafaa kufanya hivyo.

Wakaondoka na dalali. Baada ya hatua kadhaa, Chris alimwambia dalali ukweli kwamba hawajaipenda hiyo nyumba na kumpa kibarua cha kuwatafutia nyumba nyingine.

Dalali aliahidi kutafuta nyumba nyingine huku akiwaambia kwamba kwa mahitaji yao nyumba ile ilikuwa mwafaka, iko barabarani na nzuri. Joyce aliendelea kuikataa.

Siku ya pili yake, Jumamosi asubuhi, Joyce aliyekuwa ameketi kwenye kochi akisoma jarida la mambo ya urembo. Chris alikuwa amesimama katikati ya sebule akiwa amevaa nguo za mazoezi akijipanga kuanza kufanya mazoezi. Alikuwa akimshawishi Joyce akiunge naye kwenye mazoezi akasema ataanza siku nyingine.

Baadaye akamgeukia Joyce, "Hivi, honey, vitu vyote hivi (makochi, viti, meza na makabati ya vyombo) tutavipeleka wapi? Vitaenea hotelini... Ndio maana nilitaka tuichukue ile nyumba na dalali nimeongea naye anasema bado hajapata nyumba ya aina tunayotaka."

"Mimi nashauri, baadhi ya vitu kama makochi, kabati, meza na TV, tuvipeleke nyumbani kwetu, Cheyo. Vitakaa vyema tu," alijibu Joyce. Muda wowote walikuwa walimtazamia Dokta Nimrod Goima aliyechukua nyumba hiyo kama malipo ya kuficha kifo cha mkewe ili kuwasili.

Baada ya Chris kukosa pesa zilizohitajika kwa ajili ya kuficha kifo cha mkewe, Dk. Goima alimshauri ampe nyumba na yeye akawa tayari kumrudishia fedha alizokuwa ameshamtangulizia, Sh milioni 20 na kuahidi kumwongezea Sh milioni tano ambazo angezilipa kidogokidogo. Dk. Goima alikuwa amemtisha kwamba kama hampi nyumba au pesa alizotaka, basi alikuwa hana namna isipokuwa kuweka wazi kuhusu kifo cha mkewe, jambo ambalo alisema hata yeye linaweza kibarua chake rehani.

Hata hivyo, katika mjadala mkali, Dk. Goima alikubalia kumwongezea Sh milioni 10, kwani alipoiona nyumba alisema ilihitaji ukarabati.

Wakiwa bado katika mjadala wa mahala pa kuweka vyombo wakati wakisaka nyumba ya kuhamia, hodi iligongwa mlangoni. Chris aliuendea mlango kwa kusitasita. Alihisi anaweza kuwa dada yake ambaye alikuwa hajazungumza naye kwa takribani mwezi mzima wala kupokea simu yake. Alihisi kama ni dada yake angeweza akawa ameandamana na mkwewe pamoja na shemeji yake, Jacob.

Alipofungua mlango, akakutana na Dk. Goima.

"Afadhali umekuja Bwana Goima. Labda unaweza kutusaidia tatizo moja hapa. Tafadhali sana."

"Tatizo gani tena, Chris?"

"Tunaomba uturuhusu kutunza vyombo vyetu hapa kwa siku chache tu wakati tukiandaa mahali pa kuvipeleka. Na pia utupe tena siku mbili. Hatujapata nyumba. Kama hizo siku mbili zitaisha bila kupata nyumba, tutahamia hoteli."

"Hilo halina shaka kabisa," akabu Goima "Hata wiki nzima ninaweza kuwapa ya kuishi na mwezi mzima wa kutunza vitu vyenunn, lakini naombeni chonde usipite muda huo. Ninataka kubadilisha mambo mengi hapa tena haraka ili kukidhi mahitaji ya mpangaji nikiyempata," alisema Dk Goima ambaye alikuwa akiishi nyumba za serikali, jirani na hospitali ya Kitete.

"Nashukuru sana, huo muda unatutosha kabisa. Kwanza nadhani hata wiki hautaisha kama dalali atafanya kazi yake ipasavyo," alijibu Chris.

"Basi mie naondoka nilipita kuwasalimia tu, na kutaka kuwajulisha kwamba kesho ndio ninataka kuanza ukarabati. Basi ninaahirisha hadi utakavyonikabidhi ufunguo.'

"Tunashukuru sana," alijibu Chris akimshika mkono. Dk. Goima alipondoka na Chris akafunga mlango nyuma yake.

"Nyumba tutajenga nyingine tu mpenzi. Usiwe na wasiwasi. Na kwa vile umenifungulia duka la nguo na urembo, utaona mwenyewe. Miezi sita tu tunajenga nyumba nyingine," alisema Joyce akinyanyuka na kumkumbatia Chris ambaye ni kama alikuwa haamini kama nyumba ile sasa si yake tena.

***

Mwalimu Misango alikuwa mezani anamsubiri mumewe wanywe chai kisha waondoke kwenda makazini kwao. Mumewe alikuwa na kawaida ya kumpitisha mkewe kwa gari lake Shule ya Sekondari Milambo alikokuwa akifundisha na kisha kuendelea na safari yake.

Akiwa pale mezani alijikuta katika mawazo mazito kuhusu Chris. Mumewe, Jacton Misango alifika pale mezani na kugundua kwamba mkewe yuko kwenye mawazo na hadi anaketi alikuwa hajui kama keshafika pale mezani.

"Vipi unawaza nini?" Alimshitua.

"Ni kuhusu Chris. Yaani huyu bwanamdogo simwelewi kabisa."

"Amefanyaje tena?"

"Hapatikani kwenye simu, hali ya kupotea kwa Mama Kenny inazidi kuwa nzito, na yeye sijui anamtafuta mkewe ama la. Unaenda mwezi wa pili sasa. Ndugu zake sasa wanataka kwenda kumwona Mkuu wa Jeshi la Polisi... Nyumbani kwake nimeenda mara mbili lakini nyumba imefungwa. Sijui anawaza nini huyu bwana mdogo. Ninapanga kwenda kwake usiku huu saa tatu au saa nne. Utanisindikiza?"

Misango alivuta pumzi kisha anamgeukia mkewe: "Siamini kama tutamkuta kwa sababu nilipata habari zake jana sikuziamini lakini sasa naona ni kweli. Nilitaka nizifanyie utafiti kidogo kabla sijakuambia."

"Habari gani hizo, Baba Kessy?

"Chris kauza nyumba!"

"Usiniambie! Kauza nyumba? Kwa nini kauza nyumba huyu mtoto?"

"Mimi niliambiwa na jamaa mmoja rafiki yangu ambaye wamekuwa wakifahamiana na Chris siku nyingi kwa kuwa wanafanya biashara za kufanana. Naye ni mfanyabiashara."

"Siamini. Nitakwenda kuhakikisha kama imeuzwa. Sasa anaishi wapi?"

"Sijui anapoishi."

"Huyu mtoto ameingiwa na shetani gani? Lakini nilimwambia kwamba yule mwanamke atamfikisha pabaya na kweli anamfikisha kubaya kama kweli kauza nyumba... lakini siamini."

"Unasema ndugu zake wanataka kumwona Mkuu wa Jeshi polisi, kwa nini?"

"Wanaona kama polisi hapa Tabora wanawazingua katika kumbana bwanamdogo awasaudie kumpata mama Kenny. Jacob anasubiri mshahara uingie aende makao makuu Dodoma. Jana akizungumza na mimi kwa simu alisema asimpopata ushirikiano kutoka kwa mkuu wa polisi atamtafuta hata Waziri wa Mambo ya Ndani."

"Duh! Yamekuwa hayo! Kwa hiyo wanahisi Chris kamficha?"

"Wanataka awajibike zaidi. Wanaona polisi wanamchekea kwani wanaona yeye ndiye chanzo cha yote," alisema na kuongeza kwamba anaona kama wako sahihi.

*Itandelea*

# Tetemeko la ardhi laua watu 111



**BEIJING, China**

WATU 111 wameuawa na wengine 220 kujeruhiwa kufuatia tetemeko la ardhi lililotokea juzi usiku Kaskazini-Magharibi mwa Uchina, vyombo vya habari vya serikali vimeripoti.

Tetemeko hilo la kipimo cha 5.9 lilipiga Mkoa wa Gansu saa 6:00 usiku (16:00 GMT) na kuangusha majengo katika eneo hilo na Mkoa wa Qinghai upande wa Kusini.

Wafanyakazi wa dharura wanastahimili hali ya baridi kali kujaribu kusaidia watu katika eneo la mwinuko wa juu.

Tetemeko la pili lilipiga Mkoa jirani wa Xinjiang saa chache baadaye jana.

Uharibifu uliosababishwa na tetemeko hilo la kipimo cha 5.5, haujabainika.

Rais wa China, Xi Jinping, ameamuru juhudi za uokoaji katika Gansu, mojawapo ya mikoa maskini zaidi ya China.

Gansu iko kati ya Nyanda za Juu za Tibet na Loess na inapakana na Mongolia.

Tetemeko la ardhi la Jumatatu usiku lilipiga mkoa unaojisimamia wa Linxia Hui, eneo la kiutawala la Waislamu wa Hui wa China.

Utafiti wa Jiolojia wa Marekani (USGS), ulisema ulikuwa na ukubwa wa 5.9 na kina cha kilomiota 10 (maili sita).

BBC.

**VITA VYA ISRAEL, HAMAS:**

# Video yawaonesha mateka watatu wazee wa Israel

**GAZA, Israel**

MRENGO wenye silaha wa Hamas, al-Qassam, umetoa video ya wazee watatu wa Israel wanaoshikiliwa mateka katika Ukanda wa Gaza.

Video inawaonyesha Chaim Peri, 79, Yoram Metzger, 80 na Amiram Cooper, 85.

Peri anaonekana akihutubia kamera na kuomba waachiliwe.

Jumla ya mateka 120 bado wanasadikiwa kuzuiliwa mjini Gaza baada ya shambulio baya la Hamas Oktoba 7, mwaka huu.

Jeshi la Israel lilielezea kanda hiyo kama video ya uhalifu wa kigaidi.

"Tunashuhudia ukatili wa Hamas dhidi ya raia wasio na hatia, wazee ambao wanahitaji huduma ya matibabu," Daniel Hagari, Msemaji wa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) alisema.



**Kutoka kushoto kwenda kulia: Amiram Cooper, Yoram Metzger na Chaim Peri, ambao kwa sasa wanazuiliwa mateka huko Gaza.**

"Ulimwengu lazima uchukue hatua ili kutoa msaada wa matibabu na kuangalia hali ya mateka. Tunawajibika kimaadili kufanya kila juhudi ili kuwarudisha mateka nyumbani," Msemaji huyo aliongeza.

Video hiyo ilitolewa kwenye programu ya kutuma ujumbe ya Telegraph.

Mateka hao waliochukuliwa Oktoba, mwaka nhuu, wanaaminika kushikiliwa na Hamas na makundi washirika ya Wapalestina.

Wafungwa wa kivita na mateka, wanalindwa chini ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu.

Msemaji wa Kibbutz, Nir Oz, ambako watu hao walitekwa nyara, alimtaka Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, ambaye kwa sasa anazuru Israel, kufanikisha kuachiliwa huru kwa mateka hao.

"Tunashukuru kwa dalili zozote za maisha kutoka kwa mateka, lakini muda unakwenda," Msemaji huyo alisisitiza.

**VITA VYA UKRAINE:**

# Kyiv yapunguza operesheni za kijeshi

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imeonya kuwa tayari inalazimika kupunguza baadhi ya operesheni za kijeshi kwa sababu ya kupugua kwa misaada ya kigeni.

Jenerali Mkuu, Oleksandr Tarnavskyi, alisema wanajeshi wanakabiliwa na uhaba wa risasi kwenye mstari wa mbele kabisa na kusababisha tatizo kubwa kwa Kyiv.

Haya yanajiri wakati mabilioni ya Dola ya misaada ya Marekani na EU, yamezuiliwa huku kukiwa na mizozo ya kisiasa.

Ukraine ilisema inatumai kuongeza hifadhi yake ya risasi kwa usaidizi wa magharibi.

Lakini inategemea sana vifaa vya magharibi, haswa juu ya uwasilishaji wa makombora ya masafa marefu na mifumo ya ulinzi wa anga ili kupigana na majeshi ya Urusi.

Jenerali Tarnavskyi aliliambia Shirika la habari la Reuters kwamba nchi hiyo haikuwa na makombora ya mizinga, hasa kwa silaha zake za enzi ya Soviet.

"Kiasi tulichonacho hakitoshi, kwa kuzingatia mahitaji yetu," alisema na kuongeza: "Kwa hiyo tunazisambaza upya'. BBC.



# US yatangaza muungano wa kimataifa kulinda meli

**WASHINGTON, Marekani**

SERIKALI ya Marekani imetangaza muungano wa kimataifa utakaozingatia usalama katika Bahari Nyekundu, kufuatia msururu wa mashambulizi dhidi ya meli za kibiashara.

Katika taarifa yake, Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, alisema mashambulizi ya kiholela ya Houthi kutoka Yemen dhidi ya meli, yanatishia mtiririko huru wa biashara, kuhatarisha maisha ya mabaharia wasio na hatia na yanakiuka sheria za kimataifa.

Kampuni kadhaa kubwa za meli yamesitisha shughuli zake katika eneo hilo kufuatia msururu wa mashambulizi dhidi ya meli katika mlango wa Bab al-Mandab na wanamgambo wa Houthi wanaoungwa mkono na Iran katika siku na wiki za hivi karibuni.

"Bahari Nyekundu ni njia muhimu ya maji ambayo imekuwa muhimu kwa uhuru wa usambazaji na ukanda mkubwa wa kibiashara unaowezesha biashara ya kimataifa," alisema.

Njia hiyo ya meli inaunganisha meli zinazotoka Asia na Afrika Mashariki hadi Ulaya kupitia Mfereji wa Suez nchini Misri, ambao ndiyo sehemu kuu ya kufikia Bahari ya Mediterania kwa meli zinazosafiri kutoka Bahari ya Hindi.

Nchi ambazo "zinatafuta kushikilia kanuni ya msingi ya uhuru wa urambazaji", Austin anasema, lazima zifanye kazi pamoja ili kuzuia Houthis kurusha makombora ya balestiki na ndege zisizo na rubani kwenye meli za kibiashara katika maji ya kimataifa kutoka Yemen.

Aliongeza kuwa ujumbe huo uliopewa jina la Operesheni Prosperity Guardian, utajumuisha Uingereza, Bahrain, Canada, Ufaransa, Italia, Uholanzi, Norway, Ushelisheli na Uhispania.

BBC.



# Ligi ni ya Yanga na Simba tu?

MIJADALA ya ligi kuu yetu inaendeshwa kama vile ligi hiyo ina timu mbili tu za Yanga na Simba. Mjadala wa makosa kimaamuzi unaochukua siku kadhaa kuwepo kwenye media ni wa kosa lililowanufaisha au kuwaathiri Simba na Yanga.

Haina tija sana kuorodhesha matukio mengi lakini tukumbuke offside iliyokosewa Singida iliyowanufaisha Simba dhidi ya Singida nini sijui (kwa maana ya Big Stars au Fontain Gate). Juzi tena ilikuwa penalti ya Simba dhidi ya Kagera Sugar iliyorudiwa ikidaiwa kimakosa. Mjadala wake ni balaa.

Mimi ni mtazamaji zaidi wa mechi za timu nyingine zisizowahusisha Yanga na Simba. Nimeona kule Sokoine Mbeya mchezaji wa Tanzania Prisons alidakwa miguu kabisa na kipa wa Dodoma Jiji huku mpira akiwa ameshautanguliza mbele mchezaji huyo wa Prisons.

Kilichonisisimua ni kitendo cha mchezaji huyo kushangilia kwa kunyoosha ngumi juu akijua kwamba hata refarii mjinga kuliko wote duniani angetoa penalti lakini refa wetu mwenye akili nzuri aliamua iwe goal kick! Hakukuwa na mjadala wowote wa maamuzi hayo ya ajabu kama vile Tanzania Prisons wamevamia ligi kuu ya Yanga na Simba!

Azam FC walinyimwa bao dhidi ya Dodoma Jiji kule Jamhuri Dodoma kwa offside ambayo haikuwepo kabisa. Si ile ya kutangulia mguu au goti bali wachezaji wengi wa Dodoma Jiji walikuwa karibu zaidi ya lango lao kwa umbali mrefu kumfikia mchezaji wa Azam aliyedaiwa kuotea aliyekuwa mbali zaidi na lango hilo! Hii ingekuwa Simba wamenufaika hivyo, mjadala wake ungekuwa wa kutisha. Azam FC wakaonewa kimya kimya. No mjadala, no nini.

Azam FC hao hao majuzi dhidi ya JKT Tanzania hapo Chamazi, mchezaji wao akakatwa kwanja ndani ya eneo la penalti. Refa wetu mwenye akili nzuri hakuliona tukio hilo lililoonwa na wengi! Kwa nini msaidizi wake hakumsaidia? Naye hakuona? Hatujadili kabisa upendeleo huo wa wazi wazi kwa sababu hao ni Azam FC ndani ya ligi ya Yanga na Simba!

Kule Singida, timu ngeni ya Tanzania Prisons ililalamikia goli la ushindi wa 2-1 la Singida ambalo Prisons walilodai lilifungwa kwa mkono. Kwa sababu ilikuwa mechi iliyozihusisha timu zisizo Yanga na Simba, mjadala wa tukio hilo haukuwepo.

Angalau ingehojiwa kwa nini refa wetu mwenye akili nzuri hakwenda kumhoji msaidizi wake hasa ikizingatiwa msaidizi huyo hakurudi kati baada ya bao hilo? Ndiyo, hakurudi kati kwani wachezaji wa timu ya Prisons walikuwa wanamsihi refa akamuulize pale aliposimama karibu na kibendera cha kona.

Refa alihitimisha mzozo huo kwa kutoa kadi nyekundu kwa mchezaji mmoja kila upande na kuamuru mpira uwekwe kati. Yanga au Simba, wenye ligi yao wangehusika na tukio hilo, mjadala wake ungekuwa kufuru kubwa.

Hata kama Yanga na Simba wanatumika zaidi kwa habari kibiashara, tutapungukiwa nini tukijadili matukio tata ya wengine pia? Kwani ligi ni ya Yanga na Simba pekee? Hapo ndipo ninazidi kuimarisha mtazamo wangu kwamba soka kwetu si shughuli yetu rasmi bali soka kwetu ni Yanga na Simba tu.

Unabisha? Simba wakipoteza mechi moja kwa Yanga kisha wakatoka sare na Namungo, utasikia mijadala mizito mno ya kujadili udhaifu wa Simba, changamoto zake, inatakiwa ifanye nini, wachezaji vipi na benchi la ufundi vipi lakini Mtibwa Sugar iliyo mgawa points na mabao kwa wengine, nyumbani Manungu na ugenini wala haijadiliwi inavyojadiliwa Simba illiyopoteza points tano tu huku aliyepoteza points chache zaidi, Yanga, kapoteza tatu, tofauti ya points mbili tu! Tunashangaza na kusikitisha.





# Macho na masikio ya Africa katika soka kwa sasa

**Na Valensi Mbaga**

ULAYA imepambwa na baadhi ya wachezaji bora wa Kiafrika katika historia ya hivi karibuni, kutoka kwa George Weah, Samuel Eto'o hadi Didier Drogba, na wengine wengi. Bara limeendelea kutoa talanta zaidi, na kuahidi mustakabali mzuri mbeleni.

Katika makala haya, tunaangazia kwa undani wachezaji tano wa Kiafrika wakubwa duniani kote mwaka wa 2023. Kuanzia ustadi wao wa ajabu uwanjani hadi safari zao za mafanikio, wachezaji hawa wana uhakika wa kuacha alama kwenye mchezo huo mzuri kwa miaka mingi ijayo.

**5.Riyad Mahrez (Al Ahli)**

Mchezaji huyu ambae kwa sasa anaitumikia timu ya Al Ahli ya nchini Saudi Arabia ni moja kati ya waAfrika ambao wana mafaniko makubwa zaidi katika soka.

Katika kikosi chenye ushindani kama Manchester City, kupata nafasi kwenye timu inaweza kuwa kazi kubwa. Walakini, Riyad Mahrez alifanikiwa kuweka nafasi yake kwenye timu, na sio ngumu kuona kwanini.

Mchezaji huyua alikuwa na msimu mzuri 2022/23, akiwa na mabao 15 na asisti 13 katika mashindano yote 2022/23.

Michango yake ilicheza jukumu muhimu kwa upande wa Pep Guardiola kupata ushindi wa mataji matatu ya ajabu.

**4.Thomas Partey (Arsenal)**

Baada ya kuvumilia misimu michache iliyojaa majeraha huko London, Thomas Partey hatimaye alipata nafasi ya kuonyesha talanta yake uwanjani. Na kijana, alifanikiwa kufanya vema .

Kiungo huyo wa kati wa Ghana alisaidia sana Arsenal kushinda mataji , na kufanya vyema kila wiki. Partey alionekana kuwa moyo mzuri wa safu ya kiungo ya The Gunners, na mashabiki wanatarajia zaidi kwenye msimu wa 2023/24.




Victor Osimhen amekuwa na kiango bora uwanjani mnamo 2023 kipa mkongwe









**3. Sadio Mane (Al Nassr FC)**

Mane ni moja ya wanasoka bora wa Afrika na alianza polepole wakati wa msimu wake pekee katika klabu ya Bayern Munich, akihangaika kupata kiwango chake akiwa na timu hiyo.

Hata hivyo, alionekana kuwa muhimu katika kusaidia klabu kupata taji lingine la Bundesliga. Ingawa uchezaji wake mnamo 2023 haukufikia viwango vyake vya juu vya kawaida, hakuna ubishi kwamba Sadio Mane anajumuishwa katika safu ya juu ya wachezaji bora wa Kiafrika. Sasa anatimiza majukumu yake katika klabu ya Al Nassr ya Saudi Arabia.

**2. Mohamed Salah (Liverpool)**

Ikiwa wewe ni mmoja wa watu ambao bado wanafikiria Mohamed Salah ni mchezaji mwenye ubinafsi, basi unahitaji kuangalia kwa karibu takwimu zake.

Mfalme huyo wa Misri amemaliza misimu miwili iliyopita akiwa na takwimu mara mbili kwenye Ligi kuu ya England(EPL) , na hivyo kudhihirisha kuwa yeye ni mmoja wa wachezaji bora zaidi katika soka.


Hata Liverpool walipotoka kwenye reli msimu wa 2022/23, Salah alibaki bila kuzuilika uwanjani. Ingawa kumweka nafasi ya pili kati ya wachezaji bora wa Kiafrika kunaweza kuonekana kama chaguo la ujasiri, inaonyesha tu ubora kamili unaokuja kutoka barani Afrika katka soka

**1. Victor Osimhen (Napoli)**

Victor Osimhen amekuwa na kiango bora uwanjani mnamo 2023. Kwa uchezaji kama wake, haishangazi tunamweka juu ya orodha ya wachezaji bora wa Kiafrika. Hakika, wengine wanaweza kudharau uwezo wa mtu huyu i, lakini tusisahau mafanikio yake ya ajabu huko Naples.

Osimhen alichangia pakubwa katika kuiongoza Napoli kutwaa taji lao la kwanza la Serie A tangu enzi ya gwiji Diego Maradona mnamo 1990. Na ikiwa hiyo haitoshi kukuvutia, alimaliza akiwa mfungaji bora wa ligi ya Italia akiwa na mabao 26.

Kuachana na ubora wa wachezaji hao ila wapo pia vijana wadogo wanaokuja juu katika soka la Africa ikiwemo Novatus Miroshi (Shakhtar Donesk,Tanzania), Edmond Tabsoba (Leverkusen, Burkina Faso), Samuel Chukwueze (Ac milan, Nigeria), Reinildo (Atletico, Msumbiji), Habib Diallo (Strasbourg, Senegal) , Boulaye Dia (Salernitana, Senegal).



# Maneti na Usia katika mahusiano

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 1983, Hemed Manety Ulaya wa Vijana Jazz (pichani chini) alikuwa na umri wa miaka 28 ikimaanisha alikuwa na umri wa kijana wa sasa aliyezaliwa mwaka 1995.

Akiwa na umri huo na chini ya huo aliongoza kundi lililokuwa na hadhi kubwa na maarufu la Vijana Jazz Band. Alitunga nyimbo za kuburudisha sana, za kuasa na za kuelimisha. Tena mwaka huo, ungejifunza vitu vingi kuhusu mkoa wa Tanga, wa maisha yake licha ya yeye kuwa na asili ya Mkoa wa Rukwa kwa upande wa baba yake akiwa Mfipa aliyeshangaza kwa kuongea vizuri kifipa licha ya kwamba mama yake alikuwa M-mbulu na yeye alikulia mkoani Tanga!

Uzoefu unaonesha watoto wengi hujifunza zaidi lugha za mama zao. Kwenye wimbo wa Tanga hakuna kilichoachwa; wilaya zake, makabila yake, shughuli zake za uchumi na mengine huku wimbo wenyewe ukipigwa vizuri mno, Vijana Jazz wakiuliza nini maana ya jina Tanga.

Mwaka huo 1983,pamoja na wimbo huo wa Tanga na nyingine kali, kulikuwa na wimbo mmoja waliouita Ibrahim Nashangaa. Nakumbuka sauti nzito yenye mvuto ya ndugu yangu Peter Makorongo wa RTD baada ya kumaliza kusoma Salaam, "kwa upande wa burudan wanakuja Vijana Jazz na wimbo wao Ibrahim Nashangaa." kisha utawasikia kina Manety wakija hivi:-

"Enzi na enzi utani ulikuwepo, leo mimi ninashangaa" (matarumbeta)

"Mzee Bakari kapamba moto kaanza kunichapa bakora (matarumbeta)

"Hili na hili sina Ibrahim ninashanga" (matarumbeta)

"Nauliza jibu nijue baba lipi nililokukosea" (matarumbeta)


"Hili na hili sina Ibrahim ninashangaa" (matarumbeta)

Korasi wakiimba wawili wawili:-

"Itabidi ujirekebisheee kwani mimi nimeshakugundua nini nia yako."

"Mwanangu wa kike isiwe kisingizio, cha kunivunjia heshima kwa mke wangu Ibrahim."

> Uzoefu unaonesha watoto wengi hujifunza zaidi lugha za mama zao. Kwenye wimbo wa Tanga hakuna kilichoachwa; shughuli zake za uchumi na mengine huku wimbo wenyewe ukipigwa vizuri mno. Vijana Jazz wakiuliza nini maana ya jina Tanga.



Hayati Hemedi Maneti



Hemedi Maneti (kulia) akiwa na Joseph Nyerere mwaka 1989, wote kwa sasa ni marehemu



Baadaye vyombo vya kufa mtu.

**NASAHA NILIZOPEWA IBRAHIM KWA UTUNZI HUO**

Chunga sana watu wenye mambo ya kizamani wa kutania vibinti vidogo kama mchumba. Utani huo hutumika na baadhi ya watu wenye mawazo ya kishetani kupitishia mambo ya kishetani yahusuyo ngono.

Binti kama ameshafikia utu uzima, utani huo hutengenezwa kumhujumu kingono ingawa bado yuko chini ya wazazi akiwa kwenye masuala ya kielimu. Ni hatari.

Kuna waliotumia utani huo kujiweka karibu na familia ya mwanamke waliyemuwinda. Ibrahim nilitumia utani kwa familia ya Mzee Bakari kupitia utani wa uchumba kwa bintiye ili nimrubuni mke wa Mzee Bakari kimapenzi.

Mzee Bakari alikuwa mstaarabu sana kwani alinitia Bakora na kunionya nisitumie utani wa bintiye kuingilia ndoa yake. Angekuwa katili angenifanyia jambo la hatari zaidi.

Wazazi jiulizeni, mabinti wenu walipokuwa wadogo, vijana walikuwa wanapita njia tu. Sasa mabinti wamekua, eti vijana wamekuwa marafiki wakubwa wa vijana wenu wa kiume! Kuwa makini kama mabinti wenu wako sekondari kushuka chini. Mzee Bakari alinishtukia kwa maslahi ya ndoa yake na kunichapa bakora.

Miongoni mwa vitu vya kutoamini maishani ni ukaribu wa mwanamke na mwanaume wenye uhusiano wa kuweza kujamiiana. Usitoe uhuru mkubwa kwa watu wa hivyo kwa mtu anayekuhusu kama mwanamke wako au mwanaume wako.

> Kuna waliotumia utani huo kujiweka karibu na familia ya mwanamke waliyemuwinda. Ibrahim nilitumia utani kwa familia ya Mzee Bakari kupitia utani wa uchumba kwa bintiye ili nimrubuni mke wa Mzee Bakari kimapenzi.



# Urembo na tamaduni

Na Hidaya Machupa

UREMBO hauishii tu kwenye make up tu, kwa upande wa tamaduni zetu urembo huwa kwenye namna nyingi sana kutokana na makabila.

Dhana ya urembo ni ngumu kufafanua kwani urembo hutoka ndani na mara nyingi tunaambiwa uzuri upo machoni pa mtazamaji. Inakuwa changamoto zaidi kufafanua urembo wakati wa kuibua dhana mbalimbali za urembo kulingana na jamii, imani na tamaduni tofauti. Ingawa kuna tofauti kama hizo kati ya tamaduni moja na nyingine, jambo moja linaunganisha haya yote, kila moja ina sheria zake za kuamua urembo na tunagundua baadhi ya viwango vya urembo katika tamaduni tofauti.

Kabila linalotambulika kama wamakonde na wameto wanaishi katika mkoa wa Cabo Delgado kaskazini-mashariki mwa msumbiji na wamakonde wa Tanzania wanaishi zaidi mkoa wa Mtwara, wamekuwa na sifa ya kipeke yao kwenye swala la urembo.

Tofauti kubwa Kati ya wamakonde wanaoishi msumbiji na Tanzania ni aina ya urembo wa ndonya. Wale wa msumbiji Wana ndonya ndogo juu ya midomo yao Wakati wa Tanzania wanandonya kubwa zaidi mdomoni mwao.


Wamakonde huonekana kwa uzuri wao waliochanja sehemu za juu ya mdomo, masikio na uso, inaaminika kuwa chanzo cha kuchanja, kutoboa midomo na kuweka ndonya kwa ajili ya urembo. Urembo wao uliwaokoa dhidi ya wafanyabiashara enzi za utumwa kwani ndonya zao zilionekana kama ni vipele vilivyosababishwa na ugonjwa ambukizi hivyo hawakuchukuliwa kama watumwa waliachwa.

Tabia hizi zikawa ni desturi na Mila zao na zikawa kama urembo ndani ya Kabila. Mila hizi zilionekana kwa jamii nyingine kama wamasai na walizutumia sana sana wanawake(Wali) ili kuwa kivutio kwa wanaume waweze kuolewa.

Urembo huu wapo waliuacha kabisa na wengine kuendelea nao kama sehemu ya tamaduni.

Kabila la Wamasai na makabila mengine barani Afrika kwa kawaida huonekana kuwa na masikio marefu. jowl nzito zinazotengenezwa na miamba au meno ya tembo hii inaruhusu masikio kutanuka zaidi siku baada ya siku. Urembo huu,hufanywa katika makundi ya kikabila katika Afrika, inaruhusu aina ya hali kwa mwanamke, iliyosisitizwa na kiwango cha masikio marefu na mapana ambayo kufunikwa na lulu za rangi na vito.


Kwa kumalizia, utamaduni ni kipengele changamano, tofauti, na kizuri cha kuwepo kwa mwanadamu. Inajumuisha imani zetu, desturi, mila, sanaa, lugha, na kanuni za kijamii, zinazounda utambulisho wetu, mitazamo ya ulimwengu, na njia za maisha. Uanuwai wa kitamaduni ni ushuhuda wa werevu na uthabiti wa ubinadamu, na una jukumu muhimu katika kuhifadhi maarifa, kukuza ubunifu, na kukuza maelewano. Kukumbatia na kusherehekea utofauti wa kitamaduni kunaweza kusababisha ulimwengu jumuishi zaidi, wenye huruma, na wenye usawa ambapo uzuri wa urithi wetu wa pamoja wa binadamu unang'aa.







> **Tofauti kubwa Kati ya wamakonde wanaoishi msumbiji na Tanzania ni aina ya urembo wa ndonya. Wale wa msumbiji Wana ndonya ndogo juu ya midomo.**





Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Desemba 20-26, 2023 |

## Singida yajisogeza kwa Peter Banda

**Na Mwandishi Wetu**



WAKATI Dirisha dogo la Usajili limefunguliwa tayari vikumbo vimekwishaanza ili kuhakikisha kila timu inamaliza msimamo wa Ligi ikiwa kwenye hatua nzur ikama si kuwemo kwenye nne bora basi isikosekane kwenye kumi bora.

Singida FG tayari imeanza mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Peter Banda ambaye kwa sasa anaichezea Nyasa Big Bullet ya Malawi.

Banda amewahi kuchezea Orlando Pirates ya Afrika Kusini na Simba ya Tanzania.

# Salamu zao



Inatoka uk. 1

Alikuwa ni Willy Londre Onana aliyepachika magoli mawili katika dakika 36 na 38 yaliyoipa Simba pointi tatu muhimu zilizoisogeza kwenye pointi tano.

Simba ilyokuwa imara zaidi huku ikiwakosa mchezaji nyota Saido Ntibanzokiza na Sadio Kanoute, ilionekana kutawala mchezo huku kipa Ayoub Lakard akiiendelea kuonyesha ubora wake.

Matokeo hayo yametuma Salamu kwa mechi mbili zilizobaki dhidi ya Jwaneng na ASEC Mimosah.

Lakini matokeo hayo pia yanaipa Salam Dar Young Africans ambayo leo inashuka dimbani kucheza na Medeama ya Ghana.

Yanga yenye pointi mbili inahitaji kushinda mechi ya leo ili pia kufufua matumaini ya kwenda robo fainali.

Tayari Medeama wameshaonekana kupigwa na kitu kizito baada ya kulalamikia mapokezi aliyoyapata.

## Mwijage, Yusuph waondoka West Armenia

**Na Mwandishi WEtu**

KLABU ya West Armenia inayoshiriki Ligi Kuu ya nchini Armenia imevunja mikataba ya wachezaji wawili raia wa Tanzania, Yusuf Athuman na Erick Mwijage kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Yusuf alijiunga na klabu hiyo akitokea Young Africans SC ya Tanzania huku Mwijage akitokea Kagera Sugar ya Tanzania.

Nyota hao wamepewa mkono wa kwaheri baada ya Ligi Kuu ya Armenia kumalizika huku timu hiyo ikimaliza nafasi ya 8 kati ya timu 10, alama 17 katika mechi 20, ikishinda 5, sare 2 na kupoteza mechi 13.




## Ahly ndio basi tena

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Afrika, Al Ahly wamesukumizwa nje ya michuano ya klabu Bingwa Dunia kufuatia kipigo cha 2-0 dhidi ya Mabingwa wa Amerika ya Kusini (CONMEBOL), Fluminense.

Mabao ya mchezo huo yalifungwa na Jhon Arias katika dakika ya 70 huku John Kennedy akigonga msumari wa mwisho dakika 90.

Beki wa zamani wa Real Madrid, Marcelo alikuwa sehemu ya kikosi cha vigogo hao wa Brazil.

Fluminense wametinga fainali ambapo watachuana na mshindi kati ya Manchester City dhidi ya vigogo wa Japan, Urawa Red Diamonds.



## Simba, APR, Singida kundi moja

**Na Mwandishi Wetu**

MAKUNDI ya Kombe la Mapinduzi yametangaza huku kila kundi likiwa na timu 4 kwenye timu 12 zitakoshiriki Mashindano hayo yanayotarajiwa kuanza rasmi December 28, 2023 na kumalizika January 13, 2024 kwenye Uwanja wa Amaan.

**Kundi 'A'**
Mlandege, Azam FC, Chipukizi, URA.

**Kundi 'B'**
Simba SC, Jamhuri, APR na Singida.

**Kundi 'C'**
Yanga SC, Bandari, KVZ, na Vital'o

# Royal Tour yamleta Rick Ross



**Na Mwandishi Wetu**

MSANII maarufu wa Marekani, Rick Ross anatarajiwa kuja nchini mapema mwezi Januari kwa ajili ya ziara ya kitalii.

Rick mapema mwaka juzi alisema anataka kufika Tanzania ili kupanda mlima mrefu zaidi barani Afrika Kilimanjaro na juzi alipost picha yake akifanya mazoezi ya kupunguza uzito kwa ajili ya maandalizi.

"Kama nilivyoahidi Januari nitakuwa Tanzania kwa ajili ya kupanda Mlima Kilimanjaro na nimeanza mazoezi kwa ajili ya kwenda Tanzania," alisema.

Post ya Rick imekuja siku chache baada ya msanii mwingine wa Marekani, Tyrese Gibson kupost mapumziko yake Zanzibar.

Tyrese alisema kuna sehemu Afrika unaweza kusema kama hauko dunia hii kutokana na uzuri uliopo maeneo hayo huku akihashatag Zanzibar ambako alikuwa wa siku kadhaa.

Wasanii hao wamekuwa wakifurika nchini kutokana mapokeo ya filamu ya Royal Tour iliyochezwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu ambayo ilikuwa maalum kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii.